




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



ISO 9001:2015 Certified

RIPOTI KUU YA MWAKA YA UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23



MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU
WA HESABU ZA SERIKALI
MACHI 2024



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Jengo la Ukaguzi, 4 Barabara ya Ukaguzi, S.L.P. 950, 41104 Tambukareli, Dodoma. Simu ya Upepo: 'Ukaguzi' Simu: 255(026)2161200, Nukushi: 255(026)2117527, Barua pepe: ocag@nao.go.tz, Tovuti: www.nao.go.tz

Kumb.Na.CGA.319/421/01B

28 Machi 2024

Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
S.L.P 1102,
1 Barabara ya Julius Nyerere,
11400 Chamwino,
40400 DODOMA.

**RE: KUWASILISHA TAARIFA KUU YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA
HESABU ZA SERIKALI YA MWAKA 2022/23 KUHUSU
MIFUMO YA TEHAMA**

Ninayo furaha kuwasilisha taarifa yangu ya Jumla ya Mwaka kuhusu ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA kwa mwaka wa fedha 2022/23 kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, na Kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, sura ya 418.

Taarifa hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi na kupendekeza hatua za kuboresha ambazo zinalenga kukuza uwajibikaji katika ukusanyaji na matumizi ya rasilimali za umma.


Nawasilisha,

Charles E. Kichere
Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

KUHUSU OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Mamlaka

Madaraka na wajibu wa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameelezwa kwenye Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura 418



Kufanya kazi kwa uhuru na bila upendeleo

Sisi ni taasisi ya umma isiyo na upendeleo, inayotoa huduma za ukaguzi wa hali ya juu kwa wateja wetu kwa njia isiyo na upendeleo.

Kufanya kazi kwa ushirikiano

Tunathamini na kufanya kazi kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje.

Kufanya kazi kwa kuzingatia matokeo

Tunazingatia katika kufikia malengo muhimu yenye kuaminika kwa wakati, usahihi na utumizi stahiki.



Kufanya kazi kwa utaalum

Tunatoa huduma za ukaguzi za hali ya juu kwa kuzingatia maarifa ya kitaaluma, ujuzi na mbinu bora.

Kufanya kazi kwa uadilifu

Tunazingatia na kudumisha viwango vya juu vya maadili na sheria katika utoaji wa huduma za ukaguzi.

Kufanya kazi kwa ubunifu na uvumbuzi

Tunahimiza, kuvumbua, na kubuni mawazo ya kuongeza thamani kwa ajili ya kuboresha huduma za ukaguzi

YALIYOMO

ORODHA YA MAJEDWALI.....	v
ORODHA YA VIELELEZO.....	vi
UFUPISHO.....	vii
SALAMU KUTOKA KWA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI	viii
SURA YA KWANZA: UTANGULIZI.....	1
SURA YA PILI: UDHIBITI WA JUMLA WA TEHAMA.....	3
SURA YA TATU: MIFUMO YA UHASIBU	26
SURA YA NNE: MIFUMO YA MAPATO	36
SURA YA TANO: MIFUMO YA USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU NA MISHAHARA	50
SURA YA SITA: USIMAMIZI WA MIFUMO	54
SURA YA SABA: UBORESHAJI WA MIFUMO NA UENDESHAJI WA KIOTOMATIKI	58
SURA YA NANE: UFANISI KATIKA UENDESHAJI WA MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAONI	74
SURA YA TISA: HITIMISHO	80
VIAMBATISHO	84

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1: Vipengele visivyotumika kikamilifu.....	64
Jedwali 2: Huduma za taasisi zisizo kwenye mifumo ya kielelectroniki	66

ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo 1: Viwango vya ukadiriaji na vigezo.....	4
Kielelezo 2: Tathmini ya utekelezaji wa sheria za udhibiti wa jumla wa TEHAMA.....	5
Kielelezo 3: Tathimini ya utekelezaji wa taratibu katika usimamizi wa uendelezaji wa huduma za TEHAMA	8
Kielelezo 4: Tathmini ya ufuataji na uzingatiaji wa taratibu katika usimamizi wa miundombinu ya TEHAMA.....	9
Kielelezo 5: Tathmini ya utekelezaji na uzingatiaji wa taratibu katika usimamizi wa matukio ya TEHAMA	11
Kielelezo 6: Tathmini ya utekelezaji katika kufuata utaratibu wa usimamizi wa kanzidata.....	13
Kielelezo 7: Tathmini katika kufuata utaratibu wa usimamizi wa watoa huduma za TEHAMA.....	15
Kielelezo 8: Mapitio ya utekelezaji wa utaratibu katika usimamizi wa mabadiliko kwenye mifumo ya TEHAMA	16
Kielelezo 9: Tathmini ya ufuataji na uzingatiaji wa taratibu katika usimamizi wa haki za utumiaji na ruhusa zinazotolewa kwa watumiaji wa mifumo.	19
Kielelezo 10: Tathmini ya udhibiti wa mazingira ya miundombinu ya TEHAMA.....	21
Kielelezo 11: Tathimini ya manunuzi na uundaji wa mifumo ya TEHAMA	23
Kielelezo 12: Mapitio ya Utekelezaji wa utaratibu katika usalama wa taarifa	25

VIFUPISHO

Ufupisho	Jina kamili
ATMIS	Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Biashara ya Kilimo
BCP	Mpango Endelevu wa Huduma
CBMS	Mfumo wa Usimamizi wa Bajeti Kuu
CCTV	Kamera chunguzi
CFMS	Mfumo wa kusimamia taarifa za wanufaika
CIMIS	Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali
CMVRS	Mfumo wa Usajili wa Magari
CRB	Bodi ya Usajili wa Makandarasi
DRP	Mpango wa Kuokoa Maafa
ERMS	Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali
ERP	Mpango wa Rasilimali za Biashara
GovESB	Mfumo wa ubadilishanaji taarifa na kati ya taasisi.
FiRCIS	Mfumo wa Ukusanyaji Mapato ya Uvuvi
GePG	Lango la Malipo ya Kielektroniki ya Serikali
GFS	Takwimu za Fedha za Serikali
GLICA	Mfumo wa kuomba Leseni ya Michezo ya Kubahatisha na Ukaguzi
GovNET	Mtandao wa Mawasiliano Serikalini
GRN	Kumbukumbu ya bidhaa Zilizopokelewa
HCMIS	Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali Watu
iCHF-IMIS	Mfumo wa Usimamizi wa Mfuko wa Afya ya Jamii
IFMS	Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Fedha
LIMS	Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Maabara
MAJI IS	Mfumo wa Ulipaji wa Maji
MASSEMS	Mfumo wa Usalama Baharini na Usimamizi wa Mazingira
NEST	Mfumo wa Manunuzi serikalini
NPMIS	Mfumo wa Usimamizi wa Miradi ya serikali
POAS	Mfumo wa Uendeshaji wa Bandari
POS	Kifaa cha POS
PSSN-MIS	Mfumo wa Mpango wa kunusuru kaya masikini
RIMS	Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa
RRIMS	Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Reli na Barabara
SARIS	Mfumo wa Taarifa za Usajili wa Kiakademia wa Wanafunzi
SBMS	Mfumo wa Usimamizi wa Biashara ya Usafirishaji baharini
SLPS	Mfumo wa utoaji kibali Maalum cha mizigo
TAUSI	Mfumo wa Taarifa za Mapato ya Serikali za Mitaa
TOS	Mfumo wa Uendeshaji wa shughuli za Bandari
WIMS	Mfumo wa Usimamizi wa taarifa za mahali pa kazi



SALAMU KUTOKA KWA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Ninayo furaha kuwasilisha ripoti ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023, inayohusu Mifumo ya TEHAMA. Ninapenda kutambua juhudi za Serikali, zikiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kukuza uwajibikaji na uwazi katika usimamizi wa rasilimali za umma. Vilevile, ninathamini ushirikiano kutoka kwa uongozi wa taasisi zilizokaguliwa, ambao walitoa taarifa na ufafanuzi muhimu kwa ajili ya maandalizi ya ripoti hii ya ukaguzi.

Matokeo ya ukaguzi yanaonyesha mchanganyiko wa namna tofauti za usimamizi wa Mifumo ya Tehama miongoni mwa Taasisi za Serikali. Wakati baadhi ya Taasisi zimeonyesha usimamizi mzuri wa Mifumo ya Tehama, Taasisi zingine zimekabiliwa na changamoto katika kudumisha uthabiti na utendaji wa Mifumo ya Habari. Ni muhimu kwa Serikali kuingilia kati na kuhakikisha kwamba taasisi hizi zinafanya kazi kwa ufanisi na tija, zinachangia katika uchumi, na zinatoa huduma bora kwa wananchi.

Ripoti imepangwa katika sura tisa, kila moja ikichunguza kwa kina vipengele mbalimbali, vikiwemo Udhhibiti Mkuu wa Teknolojia ya Tehama, Mifumo ya Uhasibu, Mifumo ya Mapato, Mifumo ya Rasilimali Watu na Mishahara, Mifumo ya Programu na Utawala, Uboreshaji wa Mifumo na Uendeshaji wa Kiotomatiki, Ufanisi katika Uendeshaji wa Mamlaka ya Serikali Mtandaoni. Pia, Ripoti hii inabainisha maeneo ambayo taasisi hizi zinahitaji kuboresha shughuli zao na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Katika ripoti hii, nimetoa mapendekezo kuhusu jinsi ya kuongeza ufanisi wa taasisi zilizoripotiwa, kuongeza uwazi na uwajibikaji, na kukuza utawala bora. Nina imani kwamba mapendekezo haya yatakuwa na manufaa kwa Serikali na wadau wengine katika kuhakikisha utoaji wa huduma bora.

Mwisho, natoa shukrani zangu za dhati kwa wafanyakazi wa ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa jitihada zao bila kuchoka katika kutekeleza ukaguzi na kuandaa ripoti hii. Kujitolea kwao na kazi ngumu vimekuwa muhimu katika kuandaa ripoti hii, na ninashukuru kwa mchango wao.

Charles E. Kichere
Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

MUHTASARI

Utangulizi

Ripoti hii ni muhtasari wa matokeo, mapendekezo na hitimisho la mifumo ya TEHAMA katika mamlaka, idara, wakala na taasisi mbalimbali za umma Tanzania Bara kwa mwaka wa fedha unaoshia tarehe 30 Juni 2023. Lengo kuu lilikuwa kutathmini ufanisi na utoshelevu wa udhibiti wa ndani unaohusiana na teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) na mifumo ya matumizi ili kuhakikisha usahihi wa data, usiri wa taarifa na upatikanaji wa huduma.

Matokeo muhimu ya ukaguzi ni pamoja na:

(a) Udhibiti wa jumla wa TEHAMA

Tathmini ya viwango vya mfumo wa kielektroniki serikalini na utiifu wa miongozo kwa mashirika 22 (iliyofafanuliwa katika Kiambatisho II) imeonesha viwango tofauti vya mafanikio katika udhibiti wa jumla wa TEHAMA. Hususan, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB), Wizara ya Fedha (MoF) na Mamlaka ya Udhibiti wa Bima Tanzania (TIRA) zilipata alama ya juu katika maeneo mengi, huku maeneo machache yakionesha uzingatiaji wa wastani. Kinyume chake, Wizara ya Maji (MoW), Wakala Wa Usalama Na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Wakala wa Umeme Vijijini (REA), Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Shirika la Posta Tanzania (TPC) na Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA) zilipata alama za chini mfululizo katika maeneo mengi ya udhibiti wa jumla wa TEHAMA.

Uchambuzi wangu unaonesha kuwa mashirika mengi yanatekeleza ipasavyo hatua za kulinda miundombinu yao ya TEHAMA na yameweka sera na taratibu zilizo dhahiri juu ya udhibiti wa mifumo na data za TEHAMA.

Kwa upande mwingine, maeneo kama vile mpango endelevu wa huduma (BCP) na Mpango wa Kukabilia na Majanga (DRP), Usimamizi wa Mabadiliko kwenye mifumo, Usimamizi wa Matukio ya TEHAMA, Usimamizi wa Hifadhidata, na Upataji na Uendelezaji wa Programu huonesha kiwango cha chini cha kufuata miongozo. Hii inaonesha kuwa mashirika machache yanafuata mbinu bora katika maeneo haya muhimu. Hii inaweza kuwa kutokana na sababu kama vile uelewa mdogo wa umuhimu wake, ugumu katika utekelezaji au ukosefu wa rasilimali.

Tathmini inaangazia haja ya kuboreshwa kwa mbinu za usimamizi wa TEHAMA katika mashirika mengi. Ingawa baadhi walifanikiwa kufuata taratibu katika baadhi ya maeneo, wachache sana walifikia kiwango kinachohitajika katika maeneo yote ambayo inasisitiza umuhimu wa kutekeleza uboreshaji wa kina katika usimamizi wa TEHAMA. (Rejea Sura ya 2).

(b) Mifumo ya Uhasibu

(i) Kutolingana kati ya mkataba mdogo wa manunuzi na kiasi kinachohitajika

Mfumo wa Epicor katika Bohari ya Dawa (MSD) una upungufu katika kulinganisha kiasi cha andiko la manunuzi dhidi ya mahitaji halisi. Hii imesababisha kiasi cha bidhaa 287 zilizoagizwa kuwa zaidi ya mahitaji halisi, na bidhaa 3,137 zilizoagizwa na kufadhiliwa na MSD kutokuwa na mahitaji linganifu. Hii inaweza kupelekea mianya ya ubadhilifu kama vile ukisiaji wa bei holela za bidhaa au kufanya manunuzi yasiyoidhinishwa hivyo kupelekea hasara za kifedha. (Rejea Aya ya 3.4).

(ii) Mapokezi ya Vifaa bila ya kuwa na mahitaji na mkataba wa manunuzi

Katika ukaguzi wa mfumo wa Epicor katika MSD, niligundua vifaa 37 vilivyowasilishwa bila Ushahidi wa mahitaji. Vifaa hivi havikujumuishwa katika mkataba wa manunuzi (PO). Pia palikuwa na vifaa vinne vya ziada vilivyolingana na mahitaji ya MSD. Hata hivyo, hapakuwa na mkataba wa manunuzi dhidi ya vifaa hivi. Ukosefu huu wa udhibiti unaweza kusababisha matatizo kadhaa. Kwanza, vifaa vibovu vinaweza kuishia kwenye hifadhi ya mali. Pili, vifaa vinavyohitajika mara kwa mara vinaweza kuhifadhiwa vibaya. Matokeo yake, uendeshaji wa MSD unaweza kuvurugwa na bajeti yake inaweza kuyumbishwa. (Rejea Aya ya 3.5)

(iii) Bili zilizotolewa na mzabuni pasipo nyaraka ya mapokezi ya vifaa

Katika ukaguzi wa mfumo wa Epicor uliopo MSD, nilibaini bili 148 zilizoundwa bila ya nyaraka husika za mapokezi ya vifaa. Nambari za kumbukumbu za mikataba wa manunuzi, ikijumuisha nambari ya simu na toleo la tangazo, zilizoordheshwa kwenye bili hizi hazikuweza kulingana na nyaraka zozote za mapokezi zilizopo. Hii inatokana na udhibiti duni wa mfumo unaoshindwa kuunganisha bili na nyaraka za mapokezi ya vifaa. Bila GRN kuthibitisha kuwa bidhaa au huduma zilipokelewa, MSD iko katika hatari ya kulipia huduma ambayo kamwe haikupokea. (Rejea Aya ya 3.6)

(iv) Mapungufu ya mgawanyo wa majukumu katika hatua za malipo

Ukaguzi katika Wizara ya Fedha (MoF) na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) ulibaini mapungufu. Hususani, kuna ukosefu wa mgawanyo wa majukumu, kuruhusu mtu mmoja kuwajibika katika hatua nyingi muhimu kwenye mchakato wa malipo bila uangalizi wa kina. Hali hii huongeza hatari ya makosa, ubadhilifu na kuathiri uadilifu wa miamala. Masuala hayo ni pamoja na kuunda na kuidhinisha hati za malipo bila kuidhinishwa, ukosefu wa nguvu kazi waliopewa jukumu la kuidhinisha mkataba mdogo wa manunuzi na usimamizi usiofaa katika michakato ya mfumo. Kushughulikia masuala haya mara moja ni muhimu kwa usahihi wa kifedha na uwajibikaji ndani ya taasisi zote mbili. (Rejea Aya ya 3.10)

(v) MUSE inaruhusu matumizi kupita kiasi zaidi ya Bajeti Iliyotengwa

Mfumo uliruhusu kuzidi bajeti iliyoidhinishwa kwa sababu matumizi yaliyolipwa moja kwa moja na Wizara ya Fedha kwa niaba ya mashirika mengine hayakuoneshwa kiotomatiki, na hivyo kuunda salio lililoidhinishwa na kuruhusu taasisi kutumia zaidi ya mgao wa hazina. Pia, bajeti iliyotengwa kwa ajili ya mishahara ilitumika kwa gharama za ujenzi zisizoidhinishwa, kuathiri usimamizi wa fedha na mbinu bora za utoaji wa taarifa. (Rejea aya ya 3.14)

(vi) Matumizi yasiyofaa ya mfumo

Ukaguzi ulibainisha baadhi ya matukio ya matumizi yasiyofaa ya mifumo katika mashirika yote ya serikali, na hivyo kuzua hofu kuhusu uwazi wa fedha, uwajibikaji na uadilifu wa mchakato. Hususani, Wizara ya Fedha ilibainika malipo yaliyoingizwa kwenye leja ya jumla bila mikataba ya manunuzi, pia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuzalisha bili za kiotomatiki zinazozidi TZS 1.4 bilioni kupitia moduli ya "bili nyinginezo" yenye uangalizi mdogo, na ukosefu wa ufuatiliaji sahihi wa vibali vilivyolipwa kupitia moduli hiyo hiyo.

Katika hali kama hiyo, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA) pia ilitengeneza bili kwa njia ya kawaida ambazo zilipaswa kuwa za kiotomatiki, na hivyo kusababisha upotevu wa mapato. Matokeo haya yanahitaji udhibiti mkali zaidi ndani ya Wizara ya Fedha, ikijumuisha kuzuia viingilio vya mkataba wa manunuzi na kupunguza matumizi ya moduli "nyingine" kwa kuzingatia utumiaji sahihi wa mfumo ndani ya TMDA. (Rejelea aya ya 3.16)

(vii) Uingiaji pamoja na matumizi yasiyoidhinishwa katika mfumo wa Fedha

Ukaguzi wangu umebaini ukiukwaji mkubwa wa usalama katika mfumo wa fedha wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA). Katika hali moja, mtu asiyestahiki alipata kuingia kwenye mfumo na akautumia kuunda bili na hati za malipo. Mtu huyu alikosa utaalumu sahihi wa uhasibu na alipuuza taratibu za uidhinishaji zilizowekwa. Hii husababisha kuongezeka kwa hatari ya ubadhilifu lakini pia, kuna uwezekano wa kutokuwa na usahihi katika kumbukumbu za fedha (Rejea Aya ya 3.18).

(c) Udhibiti katika mifumo ya mapato

(i) Uzalishaji wa risiti nyingi kutoka kwenye malipo yaliyofanyika mara moja katika taasisi ya TSN

Mfumo wa Sage Pastel unaotumiwa na Tanzania Standard Newspapers unaruhusu malipo yaliyofanyika mara moja kutumika kutoa risiti nyingi na kutumika isivyo kulipia huduma zinginezo za wateja, ikionesha kuwa zimelipwa (Rejea Aya ya 4.3).

(ii) Ada za usajili hazijasakinishwa katika mfumo wa Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA)

Mfumo wa TMA “Integrated Weather Portal” unaotumiwa na TMA haukuunganishwa kukusanya ada za usajili kutoka kwenye vituo vya watoa huduma za hali ya hewa. Hitilafu hii inaweza kusababisha malipo yasiyo sahihi. (Rejea Aya ya 4.15)

(iii) Mapungufu ya kimgawanyo wa majukumu katika mifumo ya mapato (TASAC, TMDA, LATRA, TPA)

Ukaguzi wangu wa mifumo ya mapato katika taasisi za TASAC, TMDA, LATRA NA tpa, Ulibaini mapungufu ya udhibiti : ukosefu wa mgawanyo wa majukumu katika kuandaa bili, katika baadhi ya bili mtu mmoja alikuwa na jukumu la kutengeneza na kuidhinisha maombi mbalimbali, Mapitio yaligundua idadi kubwa ya matukio ambapo hili lilitokea, ikiwa ni pamoja na maombi zaidi ya 8,000 ya vyeti kwenye mfumo wa MASSEMS, SBMS, na TOS; maombi ya leseni za PSV katika mfumo wa RRIMS; na hata uandaji wa leseni za majaribio ya kisayansi katika mfumo wa RIMS. Ukosefu huu wa mgawanyo wa majukumu unasababishwa na udhibiti usio imara wa uhakiki wakati wa kutoa haki za uingiaji kwenye mfumo kwa watumiaji. Kwa kuruhusu mtu mmoja kushughulikia uundaji na uidhinishaji wa maombi, Hii inaongeza hatari ya makosa, na matumizi mabaya ya data. (Rejea Aya ya 4.20)

(d) Mfumo wa rasilimali watu na mishahara

(i) Mapungufu juu ya mgawanyo wa majukumu katika mfumo wa HCMIS

Ukaguzi wangu wa mfumo wa HCMIS ulibaini ukosefu wa sehemu ya kuhakiki na kutoa idhini pindi inapofanyika mabadiliko ya tarehe za kuzaliwa za wafanyakazi na taarifa za mishahara za wafanyakazi. Mtumiaji mmoja tu anaweza kubadilisha maelezo kama hayo. Hii inatokana na mfumo kutojitoshesheza katika udhibiti. Mtumiaji mmoja kutekeleza kazi muhimu za rasilimali watu huongeza hatari ya makosa na shughuli zisizoidhinishwa. (Rejea Aya ya 5.3)

(e) Usimamizi wa Mifumo ya TEHAMA

(i) Haki za utumiaji wa mifumo uliopitiliza kwa Maafisa wa TEHAMA

Ukaguzi wangu katika taasisi za serikali ulibaini kuwepo kwa hatari ya usalama wa data: utoaji haki usiofaa kwa maafisa wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Hatua hii inawapa uhuru mkubwa ambao unaweza kuhatarisha

usalama wa data na ufanisi wa uendeshaji. mifano inayotia mashaka katika taasisi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na: wafanyakazi wa TEHAMA katika mfumo wa RIMS wa TMDA ambapo maafisa hawa wanaweza kuruka hatua za uidhinishaji wakati wa usajili wa bidhaa; katika mfumo wa BCMS wa NSSF wanaweza kuunda na kufuta bili nje ya majukumu yao maalum; pia maafisa wa TEHAMA wa Ofisi ya Rais TAMISEMI walikuwa na uwezo wa kufikia katika mfumo wa TAUSI kwa njia zisizoruhusiwa. Zaidi ya hayo, Katika taasisi ya mamlaka ya serikali mtandaoni baadhi ya maafisa walipewa majukumu yasiyo stahiki (uhasibu, manunuzi, n.k.) kwa watumishi wanaofanya kazi za kutoa msaada wa kiufundi; vilevile katika Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB), Afisa TEHAMA aliingiza taarifa za wafanyakazi ambazo zinapaswa kuingizwa na afisa rasilimali watu. Ukiukwaji huu unatokana na kutokua na udhibiti wa kutosha ndani ya mfumo. (Rejea Aya ya 6.1)

(ii) Kutodhibiti uhuru wa Watoa huduma dhidi ya mfumo wa Usimamizi wa Ruzuku (Subsidy Management Systems)

Ukaguzi katika mfumo wa Subsidy Management Systems unaotumika TFRA, ulibaini kuwa mtoa huduma za TEHAMA wa nje amepewa haki za kuendelea kuingia kwenye seva na hifadhidata za taasisi kinyume na matakwa. Hii inaashiria hatari ya usalama wa data. Aidha, maafisa wa TEHAMA wa TFRA hawana uwezo wa kupakua data kutokana na vikwazo vilivyopo, Uingiaji huu wa mtoa huduma za TEHAMA wa nje unaleta hatari kubwa ya usalama wa data (Rejea Aya ya 6.3).

(f) Uboreshaji wa mifumo na uendeshaji wa kiotomatiki

(i) Ukosefu wa ujumuishaji wa Mifumo

Ukaguzi katika taasisi za serikali ulibaini kukosekana uunganishwaji kati ya mifumo mingi serikalini. Hii inatokana na ukwamishwaji wa usimamizi mzuri wa kifedha na kubadilishana taarifa kwa ufanisi. Kwa mfano, katika taasisi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF) na RFB mifumo ya kuchakata data muhimu haijaunganishwa na mifumo ya uhasibu, hivyo kupelekea kuingiza taarifa kwa mikono na kuongeza hatari ya makosa. aidha, mifumo ya malipo ya TSN, na TPDC haijaunganishwa na mifumo ya uhasibu, hivyo kupelekea kuhamisha taarifa za manunuzi kwa njia ya mikono, hivyo kuweka hatari ya uwezekano wa kutoa taarifa isiyosahihi. Upungufu huu pia uligundulika katika mifumo ya usimamizi, kama vile SPLS ya Wizara ya Ujenzi ambayo haijaunganishwa na mfumo wa TIN wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, na hivyo kusababisha makosa katika utoaji wa vibali. Ili kuboresha uwazi, ufanisi, na kupunguza makosa ya kibinadamu, nashauri uunganishwaji wa mifumo katika

taasisi za serikali, pamoja na kufanya ukaguzi wa kina wa data kwa taasisi kama OSHA na TMDA. (Rejea Aya ya 7.3)

(ii) Urudufu wa Mifumo unazuia ufanisi wa Serikali mtandaoni

Ukaguzi wangu ulionesha kuwepo kwa uanzishwaji wa miradi ya Teknolojia ya Habari na Mifumo ya TEHAMA rudufu katika taasisi mbalimbali. Mifano ni pamoja na: Bodi ya Michezo ya kubahatisha ambayo inatumia mifumo ya ERMS na Sage Pastel katika kazi za kihasibu; NSSF ambayo imeunda Mfumo wa usimamizi wa mali zake, pamoja na mfumo wa Oracle ERP iliyopo; Shirika la Posta Tanzania linatumia MUSE pamoja na Sage Pastel katika kazi za kihasibu; na Mamlaka ya Bandari Tanzania ina POAS iliyoboreshwa lakini ilianzisha zabuni ya TOS ambazo zote zinafanya kazi moja. Kwa kuongezea ERMS ya Mamlaka ya Serikali Mtandao inabaadhi ya moduli zinazofanya kazi sawa na zile zilizo katika mifumo ya HCMIS na NEST katika maeneo mbalimbali. Kutumia mifumo mingi katika kufanya kazi ya aina moja inatokana na udhhibiti mdogo wa uundaji wa mifumo na hupelekea uwezekano wa kukosekana kwa usahihi wa data katika mifumo hiyo. (Rejea Aya ya 7.6)

(g) Ufanisi wa utendajikazi wa Mamlaka ya Serikali mtandao

(i) Ucheleweshaji wa utoaji wa huduma ya barua pepe Serikalini

Maombi ya huduma za barua pepe ya serikali yaliyowasilishwa na taasisi za umma yalicheleweshwa kati ya siku 24 hadi 132, zikizidi muda uliopangwa wa kutoa huduma zinazohusiana na mfumo wa Barua wa Serikali (GMS) ambao ni ndani ya siku 3 za kazi baada ya kupokea maombi kama ilivyoainishwa katika Kipengele na 5.3 cha Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa e-GA. Ucheleweshaji katika utoaji huduma unaweza kuharibu sifa ya e-GA kama mtoa huduma anayeaminika na mwenye ufanisi kwa taasisi za umma ambazo zinaweza kuiona Mamlaka hiyo kwa mtazamo hasi. (Rejea Aya ya 8.5)



SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

Ripoti hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi wa taasisi mbalimbali za serikali nchini Tanzania, uliolenga kutathmini utekelezaji wa mkakati wa serikali mtandao na jukumu la Wakala wa Serikali Mtandao (eGA) katika kusimamia utekelezaji wake. Ukaguzi huu ulijumuisha ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA ya taasisi 57, ambapo 35 zilifanyika kama sehemu ya ukaguzi wa fedha na 22 zilikuwa kaguzi zinazo jitegemea. Lengo la ripoti hii ni kutaarifu umma kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa serikali mtandao, kutambua changamoto zozote zilizokutwa, na kutoa mapendekezo ya kuboresha utekelezaji. Ripoti hii pia inaangazia jukumu la eGA katika kusaidia taasisi za serikali kutekeleza juhudi za serikali mtandao na kuongeza utoaji wa huduma kwa wananchi.

1.0 Malengo ya Ukaguzi

Lengo la ukaguzi huu lilikuwa kutathmini manufaa na utendaji wa mifumo ya TEHAMA katika kusaidia taasisi za serikali kufikia malengo yao. Ukaguzi ulitathmini vipengele mbalimbali vya mifumo, vikiwamo: (a) Kutathmini ufanisi wa udhibiti wa mifumo ya matumizi ya serikali (b) Kuchunguza udhibiti wa jumla unaozunguka mifumo na uendeshaji wa TEHAMA; na (c) Kutathmini ufanisi wa usimamizi wa miradi ya TEHAMA.

1.1 Mawanda ya Ukaguzi

Ukaguzi wangu ulijumuisha tathmini ya mifumo ya TEHAMA inayotumiwa na taasisi za serikali. Pia, niliangalia udhibiti wa mifumo inayotumika katika taasisi, udhibiti wa jumla wa teknolojia ya habari, usimamizi wa miradi ya TEHAMA, na ufanisi wa uendeshaji wa Mamlaka ya Serikali Mtandao. Kwa mwaka wa fedha 2022/23, nilifanya jumla ya kaguzi za mifumo 57, ambapo kaguzi 35 zilifanyika kama sehemu ya kaguzi za kifedha na kaguzi 22 zilifanyika kama kaguzi za mifumo zinazojitegemea. Matokeo ya kaguzi zilizofanyika ni kwa mujibu wa kiwango cha rekodi, nyaraka, na taarifa zilizopatikana wakati wa ukaguzi

1.2 Mbinu za Ukaguzi

Ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA ulifanyika kwa kufuata viwango vya kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi (ISSAI) vilivyotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi Kuu za Ukaguzi (INTOSAI). Katika kutekeleza kaguzi hizi, nimehakikisha kwamba nafuata taratibu zilizopo za kiukaguzi, ikiwamo Mwongozo wa Ukaguzi wa Teknolojia ya Taarifa wa AFROSAI E, viwango na miongozo ya Mamlaka ya Serikali Mtandao, COBIT 5, na Mwongozo wa Kimataifa wa usimamizi wa usalama wa taarifa ISO/IEC 27001.

Njia yangu ya ukaguzi imezingatia mambo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na ufanisi na usalama wa mifumo na taratibu za TEHAMA. Nilitathmini hatari zinazohusiana na mifumo ya TEHAMA na kutambua hatua za udhibiti zilizotekelezwa ili kupunguza hatari hizi.

UDHIBITI WA JUMLA WA TEHAMA

2.1 Utangulizi

Udhibiti wa jumla wa TEHAMA (ITGCs) ni kanuni zinazosaidia kuhakikisha mifumo ya TEHAMA ya taasisi ipo salama, inaweza kufanya kazi kwa urahisi, na taarifa zinazozalishwa nizenye kuaminika. Udhibiti huu unajumuisha mambo kama kuhakikisha watu sahihi pekee ndio wanaweza kuingia kwenye mfumo, kuwepo kwa nakala rudufu iwapo janga linaloathiri miundombinu ya TEHAMA litatokea, na kwamba mabadiliko yoyote kwenye mfumo yanafanywa kwa kufuata taratibu na kwa usahihi. Udhibiti huu auhusu kazi au michakato maalum, bali unahusu mazingira kwa ujumla yanayozunguka mifumo ya TEHAMA.

Wakati wa ukaguzi wa udhibiti wa TEHAMA (ITGCs) katika sekta ya umma, lengo ni kuhakikisha kuwa mifumo ya TEHAMA ya serikali inafanya kazi kama inavyopaswa. Hii inamaanisha kwamba nakagua mifumo ili kuhakikisha kuwa mifumo ni salama, yenyekuaminika, na inatumika kwa usahihi. Ukaguzi pia unaangalia kama mifumo hiyo inaisaidia serikali kufuata sheria na kanuni zote kama vile Sheria na miongozo ya Mamlaka ya Serikali Mtandaoni. Kwa kufanya tathmini hizi, nasaidia kupunguza vihatarishi vinavyoweza kupelekea matatizo kama kupoteza data na kuhakikisha kuwa serikali inaweza kutoa huduma kwa ufanisi.

Wakati wa ukaguzi wangu wa ufanisi wa udhibiti wa jumla wa TEHAMA kwenye taasisi za umma, nilitumia muundo wa Tathmini ya utekelezaji wa sheria za udhibiti wa jumla wa TEHAMA ambao una maeneo 11 muhimu. Maeneo haya ni pamoja na usimamizi wa TEHAMA, mpango wa uendelezaji wa huduma za TEHAMA (BCP) na Mipango wa Kukabiliana na Maafa (DRP), Usimamizi wa Mtandao, Usimamizi wa matukio ya TEHAMA, Usimamizi wa kanzidata, Usimamizi wa watoa huduma za TEHAMA, Usimamizi wa Mabadiliko kwenye mifumo ya TEHAMA, usimamizi wa utoaji haki na ruhuza za utumiaji wa mifumo ya TEHAMA, Usimamizi wa miundombinu ya TEHAMA, Ununuzi na uundaji wa mifumo ya TEHAMA, na Usalama wa taarifa.

Ukaguzi wangu ulilenga kutathmini kiwango cha jumla cha utekelezaji kwenye maeneo haya dhidi ya Sheria, miongozo, na viwango vya Mamlaka ya serikali mtandaoni, na mazoea bora yaliyowekwa na ISO 27001. muundo huu wa tathmini unafafanua viwango vitano vya utekelezaji wa sheria za udhibiti wa



jumla wa TEHAMA, viwango hivyo vina anzia sifuri hadi tano (kama ilivyoelezwa kwenye Kielelezo 1).

Kulingana na muundo, Taasisi za serikali zinapaswa kujitahidi kufikia angalau kiwango cha 3 cha utekelezaji au zaidi katika maeneo yote.

Kielelezo 1: Viwango vya ukadiriaji na vigezo





2.2 Tathmini ya utekelezaji wa sheria za udhibiti wa jumla wa TEHAMA

2.2.1 Usimamizi wa TEHAMA


Usimamizi wa TEHAMA ni mfumo wa kimuundo unaosaidia taasisi kulinganisha mpango mkakati wao wa TEHAMA na malengo yao kwa kuzingatia upimaji wa utendaji na mawasiliano ya wazi. Inajumuisha maeneo muhimu kama jumla ya kazi za idara ya TEHAMA, viashiria muhimu vya utendaji kazi (KPIs), na kupima thamani ya uwekezaji wa teknolojia.

Ukaguzi wa usimamizi wa TEHAMA uliangalia mambo kadhaa, ikiwa ni pamoja na:

- Jinsi kamati tendaji ya TEHAMA, ambayo inasimamia kazi za TEHAMA, inavyofanya kazi.
- Majukumu ya watumish wa TEHAMA
- Sera za TEHAMA zilizoidhinishwa
- Jinsi ukaguzi wa ndani wa TEHAMA unavyofanyika.
- Taratibu za kuandaa bajeti ya TEHAMA
- Jinsi mpango mkakati wa TEHAMA, unavyolingana na malengo ya taasisi.

Ukaguzi pia uliangalia jinsi taasisi 22 za umma zilivyokuwa zinafuata sheria, viwango na miongozo ya mamlaka ya serikali mtandaoni katika usimamizi wa TEHAMA. viwango vya taasisi katika ufuataji wa sheria na muongozo vinaoneshwa kweye **Kielelezo Na. 2**.

Kielelezo 2: Tathmini ya utekelezaji wa sheria za udhibiti wa jumla wa TEHAMA



Nilikagua usimamizi wa TEHAMA kwenye taasisi 22 na kuona maeneo kadhaa yakuboreshwa kama ifuatavyo:

(i) Kamati tendaji za TEHAMA zisizo na ufanisi

Ukaguzi kwenye tasisi 22 kwa mwaka wa fedha 2022/23 umebaini kuwa kamati tendaji za TEHAMA za taasisi 11 zinachangamoto hizo.

- Kukosekana kwa kamati tendaji ya TEHAMA
- Kushindwa kukutana kama inavyoshauriwa

Kwa kuzingatia jukumu muhimu la Kamati tendaji ya TEHAMA katika kusimamia mipango ya TEHAMA, ambayo inajumuisha kukagua na kutoa mwongozo kuhusu uwekezaji wa TEHAMA na vipaumbele vyake, pamoja na kuhakikisha uwekezaji wa TEHAMA unaendana na mahitaji ya taasisi. Taasisi zinapaswa kuhakikisha kamati tendaji za TEHAMA zinaundwa na kutekeleza majukumu yake.

(ii) Kukosekana kwa uwiano na ufuatiliaji mdogo juu ya mpango mkakati wa TEHAMA

Kati ya taasisi 22 zilizokaguliwa, 13 zinakabiliwa na changamoto katika kulinganisha uwekezaji wa TEHAMA na malengo ya taasisi. Mikakati yao ya



TEHAMA inatofautiana na mipango ya Taasisi, na haina utaratibu mzuri wa ufuatiliaji. Changamoto hii inazuia ufanisi wa rasilimali na kuzuia teknolojia kusadia malengo ya taasisi inavyotakiwa. Ufuatiliaji wa mara kwa mara wa mpango mkakati wa TEHAMA ni muhimu kuzuia kutofautiana kwa mpango wa TEHAMA na malengo ya taasisi, kuepuka upotevu wa rasilimali na kuhakikisha maendeleo.

(iii) Kutofanyika kwa Ukaguzi wa ndani wa TEHAMA

Ukaguzi pia uligundua kwamba taasisi sita hazikufanya ukaguzi wa ndani wa TEHAMA, ikionesha uwezekano wa kushindwa kushughulikia vihatarishi vinavyohusiana na michakato inayotegemea TEHAMA kwa ufanisi. Ukaguzi wa ndani wa TEHAMA ni muhimu ili kuhakikisha udhibiti unaohusiana na TEHAMA ni wenye ufanisi, na unakidhi matakwa ya kanuni na sheria.

2.2.2 Mpango endelevu wa huduma na mpango endelevu wa kukabiliana na maafa

Katika ulimwengu wa leo ambao unaendelea kwa kasi na ambao umeunganika kwa kiasi kikubwa, taasisi lazima ziwe tayari kwa matukio yasiyotarajiwa ambayo yanaweza kuvuruga shughuli zao. Mikakati miwili muhimu ambayo husaidia kuhakikisha maandalizi haya ni Mpango endelevu wa Huduma (BCP) na Mpango wa Kudhibiti Maafa (DRP).


BCP ni mpango wa kuchukua hatua za mapema ambao huwezesha taasisi kuendeleza shughuli muhimu wakati wa, pamoja na baada ya, janga kutokea. Ni kuhusu kuhakikisha kuwa majukumu ya taasisi yanaweza kuendelea baada ya janga kutokea, kupunguza athari kwenye utoaji huduma, kwa wateja, na kwa wadau.

Wakati BCP inahusu kuendeleza shughuli za biashara, DRP inazingatia kurudisha shughuli katika hali ya kawaida. DRP ni maagizo ya kina ya kurejesha na kulinda miundombinu ya TEHAMA wakati wa janga. Ingawa Mpango endelevu wa biashara (BCP) na mpango wa Kukabiliana na Maafa (DRP) zinafanya kazi kwa malengo tofauti, zina uhusiano wa karibu na mara nyingi hufanya kazi kwa pamoja. Pamoja, zinajenga mkakati wa kushikamana wa kulinda dhidi ya changamoto za utulivu na uendelezaji wa shughuli.

Nilikagua taasisi 22 kwa lengo la kupima ufuataji wa sheria na miongozo ya mamlaka ya serikali mtandaoni kwenye taasisi hizo katika kipengele cha Mpango Endelevu wa Huduma (BCP) na Mpango wa Kudhibiti Maafa (DRP). Kilelezo Na.3

kinaonesha ni kwa namna gani taasisi zinajiandaa kuendelea kutoa huduma za mifumo wakati wa majanga.

Kielelezo 3: Tathimini ya utekelezaji wa taratibu katika usimamizi wa uendelezaji wa huduma za TEHAMA



Nilifanya ukaguzi wa Mpango Endelevu wa Huduma (BCP) na Mpango wa Kukabiliana na Maafa (DRP) kwenye taasisi 22 na kugundua yafuatayo:

(i) Kuwepo kwa mapungufu katika Mpango Endelevu wa Huduma na Kukabiliana na Majanga

Ukaguzi wangu katika Taasisi 22, nilibaini kwamba taasisi 10 hazikuwa na Mpango ya Kudumu ya Huduma (BCP) na Mpango ya Kukabiliana na Maafa (DRP). Kutokuwepo kwa mipango hiyo kunasababisha wasiwasi juu ya uwezo wao wa kuendelea na utoaji wa huduma kwa ufanisi wakati majanga yanapotokea. Ni muhimu kwa taasisi hizi kuandaa nyaraka kamili za BCP na DRP ili kupunguza hatari na kuhakikisha huduma zinaendelea kutolewa wakati na baada ya janga kutokea.

Taasisi hizi zinapaswa kutoa kipaumbele kwenye utengenezaji wa nyaraka hizi. Ili kuboresha udhibiti wao wa kuhakikisha huduma zinaendelea kutolewa wakati na baada ya janga kutokea.



(ii) Kutokufanyika juu ya majaribio ya mipango endelevu ya huduma (BCP) na mipango ya kukabiliana na maafa (DRP)


Ukaguzi wangu katika taasisi 22, niligundua kwamba taasisi 12 hazikufanya majaribio ya BCP na DRP. Hii ilitokana kukosa uchambuzi wa athari za biashara na kutokuwa na Kiwango cha muda na taarifa ambazo taasisi inaweza vumilia kupoteza. Kutokuwepo kwa majaribio haya kunaleta wasiwasi juu ya utayari wa taasisi kukabiliana na janga litakalotokea. Majaribio ya mara kwa mara ni muhimu sana kuthibitisha ufanisi wa hatua za BCP na DRP na kuhakikisha uwiano na malengo yaliyowekwa ya kukabiliana ya majanga. Kukabiliana na changamoto hii, kutaimarisha sana na maandalizi ya taasisi hizi.

2.2.3 Usimamizi wa miundombinu ya TEHAMA

Katika ukaguzi wa Usimamizi wa miundombinu ya TEHAMA, nilifanya tathmini ya ufanisi na usalama wa miundombinu hiyo. Miundombinu ya TEHAMA ni pamoja na vifaa, programu, itifaki za usalama, na njia za uingiaji katika mfumo kwa watumiaji. Lengo langu lilikuwa kutambua matatizo yaliyopo kwenye miundombinu, hatari za usalama, na maeneo ya kuboresha kwa kuchunguza muundo, mpangilio, na itifaki za mtandao.

Nilifanya kaguzi katika taasisi 22 za serikali ili kuhakikisha kama zinafuata taratibu zilizowekwa na serikali mtandao juu ya usimamizi wa miundombinu ya TEHAMA. Kiwango cha jumla cha taasisi hizi katika kufuata taratibu (compliance level) kimeoneshwa katika Kielelezo Na. 4.

Kielelezo 4: Tathmini ya ufuataji na uzingatiaji wa taratibu katika usimamizi wa miundombinu ya TEHAMA



Katika ukaguzi wa usimamizi wa mtandao kati ya taasisi 22, masuala kadhaa yalibainika. Ninawasilisha masuala muhimu katika aya zifuatazo:

(i) Kutofanya ufuatiliaji wa ufanisi wa miundombinu ya TEHAMA

Nilikagua taasisi 22 na kugundua kwamba nane kati yao hawafuatilii kujua utendaji kazi wa miundombinu ya TEHAMA, jambo ambalo linaweka usalama na utendaji wa miundombinu hii hatarini. Kwa ajili ya utendaji bora, kutatua matatizo, na kuboresha usalama na uzoefu wa mtumiaji, ni muhimu sana kwa taasisi hizo kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara wa mitandao yao.

(ii) Kutodhibitiwa kwa upatikanaji wa mtandao kwa njia ya mbali

Katika ukaguzi wangu, niligundua kwamba taasisi nne zimeacha uhuru kwa watumiaji kupata huduma za mtandao kwa njia ya mbali bila sera au taratibu zilizoidhinishwa. Mienendo hii inaongeza hatari ya ufikiaji usioidhinishwa na uvujishaji wa data. Ili kulinda usiri wa data na kuhifadhi uadilifu wa miundombinu ya mtandao ya shirika, ni muhimu kwa taasisi kuweka sera na taratibu zitakazotoa muongozo wa upatikanaji wa mtandao kwa njia ya mbali.

(iii) Kutokufanya tathmini ya uchunguzi wa usalama wa mtandao

Wakati wa ukaguzi wangu, nilibaini kuwa taasisi tatu hazikufanya tathmini ya uchunguzi wa usalama wa mtandao. Kushindwa kufanya tathmini ya uchunguzi wa usalama wa mtandao kunaziweka taasisi katika hatari ya kutotambua


mapungufu yaliyopo kwenye mitandao yao na mifumo yao ya TEHAMA, jambo linaloweza kuathiri usalama wa taarifa kwa ujumla. Ili kugundua na kutatua mapungufu ya mtandao kwa wakati, taasisi zinapaswa kufanya uchunguzi wa usalama wa mtandao mara kwa mara.

2.2.4 Usimamizi wa matukio ya TEHAMA

Usimamizi wa matukio ya TEHAMA unahusisha kuwepo kwa taratibu zinazofuatwa kwa ajili ya kushughulikia matatizo ya huduma za TEHAMA yanayoripotiwa na watumiaji wa mifumo. Lengo likiwa ni kurejesha huduma kwa haraka na ndani ya viwango vya ubora vinavyokubalika (SLA). Ukaguzi wa usimamizi wa matukio ya TEHAMA ulisisitiza umuhimu wa utatuzi wa matukio kwa wakati unaofaa ili kupunguza athari kwa watumiaji. Aidha, ukaguzi huu unapendekeza uwepo wa ukaguzi wa mara kwa mara juu ya matukio ya TEHAMA ili kuboresha ufanisi wa usimamizi wa matukio hayo na uwepo wa makubaliano ya kiwango cha Uendeshaji (OLA) kati ya TEHAMA na taasisi husika, ili kufafanua viwango vya huduma vinavyotarajiwa kutolewa na TEHAMA.

Nilifanya ukaguzi katika taasisi 22 za serikali ili kuhakikisha kama zinafuata taratibu zilizowekwa na serikali mtandaoni juu ya usimamizi wa matukio ya TEHAMA. Kiwango cha jumla cha taasisi hizi katika kufuata taratibu (compliance level) kimeoneshwa katika Kielelezo Na. 5

Kielelezo 5: Tathmini ya utekelezaji na uzingatiaji wa taratibu katika usimamizi wa matukio ya TEHAMA





Katika ukaguzi wa usimamizi wa matukio ya TEHAMA, yafuatayo ni matatizo yaliyobainishwa:

(i) Kukosekana kwa taratibu za usimamizi wa Matukio ya TEHAMA

Ukaguzi ulibainisha kuwa taasisi tano hazina sera na taratibu za usimamizi wa matukio ya TEHAMA. Hii ikiwa ni ishara muhimu ya ukosefu wa uwezo wa taasisi kujibu matukio ya TEHAMA kwa ufanisi. Ili kutoa mfumo wenye muundo wa kushughulikia matukio kwa ufanisi, taasisi zinapaswa kuanzisha taratibu za usimamizi wa matukio ya TEHAMA.

(ii) Kukosekana kwa makubaliano ya uendeshaji wa huduma za TEHAMA (OLA)

Ukaguzi ulibainisha kuwa taasisi tano hazina mikataba ya makubaliano ya uendeshaji kati ya idara za TEHAMA na idara zingine katika taasisi hizo, hii ikiwa inazua wasiwasi kuhusu uratibu, mawasiliano, na ufanisi katika usimamizi wa matukio ya TEHAMA. Ili kuwa na majukumu, wajibu, na uwajibikaji ulioelezwa wazi kati ya idara ya TEHAMA na idara zingine, taasisi zinapaswa kuunda makubaliano ya uendeshaji kwani ni muhimu kuwa na majukumu yaliyofafanuliwa.

(iii) Ucheleweshaji katika kushughulikia matukio ya TEHAMA

Ukaguzi ulibainisha kuwa taasisi nne zinachelewesha utatuzi wa matukio ya TEHAMA, zikienda kinyume na muda uliokubaliwa wa utatuzi ulioainishwa katika mikataba ya makubaliano ya uendeshaji kati ya idara za TEHAMA na idara zingine katika taasisi hizo. Ucheleweshaji huu unaathiri sio tu ufanisi wa usimamizi wa matukio ya TEHAMA, bali pia unasababisha kuchelewesha shughuli za kiutendaji za taasisi husika. Ili kushughulikia ucheleweshaji katika kutatua matukio ya TEHAMA, taasisi zinapaswa kuongeza rasilimali zinazohitajika, kutoa mafunzo kwa wafanyakazi katika usimamizi wa matukio ya TEHAMA, na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuboresha daima huduma.


2.2.5 Usimamizi wa kanzidata

Ufanisi katika Usimamizi wa kanzidata ni muhimu katika kuhakikisha usalama na utimilifu wa taarifa za taasisi zilizohifadhiwa katika kanzidata. Hii usaidia kupunguza hatari kama vile kupata taarifa kwa njia isiyoidhinishwa na uvujaji wa data. Ili kuzuia mashambulizi ya kimtandao yanayoweza kutokea na kuhakikisha usiri, upatikanaji, na utimilifu wa taarifa nyeti, taasisi lazima zisimamie kanzidata zake ipasavyo.

Nilifanya tathmini ya uchambuzi wa usanikishaji wa kanzidata (*database configurations*) katika ufuatiliaji wa shughuli za watumiaji katika mifumo. Niliangalia kama kanzidata ilikuwa inafanya kazi kwenye toleo lililoboreshwa. Pia, nilihakiki kama utambulisho wa watumiaji wa kanzidata, usimamizi wa nywila (passwords) na usimamizi wa akaunti za awali zinazokuja na kanzidata (*default accounts*) unazingatiwa kwa ajili ya usalama wa kanzidata.

Nilikagua uzingatiaji wa utaratibu katika kutekeleza usimamizi wa kanzidata kulingana na viwango na miongozo ya Serikali Mtandaoni kwenye taasisi 22 za umma kama inavyoneshwa katika Kielelezo Na. 6.

Kielelezo 6: Tathmini ya utekelezaji katika kufuata utaratibu wa usimamizi wa kanzidata



Katika tathmini ya usimamizi wa kanzidata kwenye taasisi 22 za umma, matatizo yafuatayo yalibainika:

(i) Mapungufu katika usimamizi wa shughuli kwenye kanzidata

Katika ukaguzi wa mwaka wa Fedha wa 2022/23, niligundua kuwa taasisi 16 kati ya 22 hazikuwa zimesakisha kanzidata kuweka kumbukumbu ya shughuli



zinazofanyika katika mifumo na pia hazikuwa zimefanya mapitio ya mara kwa mara ya shuguli hizo.

Upungufu huu huleta uwezekano wa kushindwa kutambua shughuli haramu zinazoendelea katika kanzidata na mifumo ya TEHAMA kwa ujumla na kuongeza hatari ya uvunjaji wa usalama wa mifumo na uadilifu wa data.

Napendekeza taasisi kushughulikia suala hili kwa kusanikisha kanzidata ili ziweze kuweka kumbukumbu za shughuli zote zinazofanyika na kufanya mapitio ya mara kwa mara ya shuguli hizo na kuanda ripoti.

(ii) Uwepo wa akaunti za awali kwenye kanzidata

Katika ukaguzi, niligundua kwamba kati ya taasisi 22 zilizokaguliwa, nane zilikuwa zinahifadhi akaunti za mtumiaji wa awali zinazokuja na kanzidata. Akaunti hizi pamoja na nywila zake, zinaweza kuleta hatari ya usalama wa kanzidata na zinaongeza uwezekano wa matumizi yasiyoidhinishwa ikiwa hazibadilishwi au kufutwa.

(iii) Matumizi ya matoleo ya zamani ya kanzidata

Kati ya taasisi 22 zilizokaguliwa, tatu zilikuwa zinatumia matoleo ya zamani ya kanzidata. Upungufu katika usimamizi na udhibiti wa matumizi ya matoleo ya kanzidata unaziweka taasisi katika hatari ya matumizi ya programu za zamani. Hali kama hiyo inaweza kusababisha mapungufu ya usalama wa mifumo ya TEHAMA na ukosefu wa msaada kutoka kwa watoa huduma, hivyo kuathiri ustawi na usalama wa mazingira ya TEHAMA kwa ujumla. Taasisi zinapaswa kusanikisha mifumo yao ya usimamizi wa kanzidata hadi kwenye toleo jipya lililopo.

2.2.6 Usimamizi wa watoa huduma za TEHAMA

Usimamizi wa watoa huduma za TEHAMA ni muhimu kwa taasisi zianazotegemea huduma hizo kutoka kwa watoa huduma wa nje. Ili kuleta ufanisi na utekelezaji kwa watoa huduma hao. Uwepo wa mahusiano kati ya mtoa huduma wa nje na taasisi unaweza kuhatarisha usalama wa mifumo ya taasisi kwa njia ya mtandao. Kuzuia athari hizi ni muhimu kuwa na usimamizi kwa watao huduma hao.

Katika ukaguzi wa taasisi 22, nilihakiki uwepo wa mikataba na makubaliano ya viwango vya huduma kati ya taasisi na watoa huduma za TEHAMA. Pia, nilifanya tathmini ya usimamizi wa huduma hizo na mabadiliko yanayoweza kutokea kwenye utoaji wa huduma hizo. Tathmini hizi zilifanyika kulingana na miongozo

ya serikali mtandaoni kwenye usimamizi wa watoa huduma za TEHAMA. Matokeo ya ukaguzi yanaoneshwa kwenye **Kielelezo Na. 7.**

Kielelezo 7: Tathmini katika kufuata utaratibu wa usimamizi wa watoa huduma za TEHAMA



Katika ukaguzi wa usimamizi watoa huduma za TEHAMA, nilibaini mapungufu yafuatayo:

(i) Kutokuwepo kwa mikataba na makubaliano ya viwango vya huduma kati ya taasisi na wauzaji wa TEHAMA

Katika ukaguzi wa taasisi 22, nilibaini kuwa taasisi 12 zinaendesha shughuli zake na watoa huduma za TEHAMA bila mikataba rasmi au makubaliano ya viwango vya huduma. hali hii inaziweka taasisi katika hatari ya kutokuwa na makubalionao rasmi ya masharti ambayo mtoa huduma anatakiwa katika kipindi amabcho anatoa huduma zake kwa taasisi husika. Pia, inaweza kuathiri ubora wa huduma zitolewazo. Napendekeza taasisi kuweka mikataba rasmi na makubaliano ya viwango vya huduma kwa huduma zote zinazotolewa na watoa huduma wa nje ya taasisi hizo.

(ii) Kutofuatilia utendaji kazi wa watoa huduma za TEHAMA

Nilibaini kuwa kati ya taasisi 22 zilizokaguliwa, 11 hazikuwa zikifuatilia utendajikazi wa watoa huduma za TEHAMA. Kutofanya ufuatiliaji wa


utendajikazi huo kunaweza kuathiri ubora wa huduma na utekelezaji wa utaratibu wa utoaji wa huduma hizo. Ili kuhakikisha huduma hizo zinakuwa bora kulingana na mikataba na makubaliano ya viwango, taasisi zinatakiwa kufuatilia utendaji wao kazi mara kwa mara na kuandaa ripoti.

2.2.7 Usimamizi wa mabadiliko kwenye mifumo ya TEHAMA

Usimamizi bora katika kufanya mabadiliko kwenye mifumo ya TEHAMA ni muhimu kwa utekelezaji uliodhibitiwa. Maboresho yasiyodhibitiwa yanaweza kuleta hatari kwa ustawi na usalama wa mfumo na taarifa za taasisi kwa ujumla. Katika ukaguzi wa 2022/23, nilihakiki uzingatiaji wa taratibu na miongozo katika kufanya mabadiliko kwenye mifumo ya TEHAMA., Tathmini hii ilijumuisha taratibu na miongozo iliyowekwa, mabadiliko yaliyoidhinishwa kwenye mfumo, mapitio baada ya utekelezaji wa mabadiliko, na utenganishaji wa mazingira ya kujenga, kufanya majaribio, na uzalishaji wa mifumo.

Nilifanya tathmini kwa taasisi 22 kwa viwango vya Serikali Mtandaoni na miongozo ya usimamizi wa mabadiliko kwenye mifumo ya TEHAMA. Kiwango cha jumla cha ufuatiliaji huu kinaoneshwa kwenye **kielelezo Na. 8**.

Kielelezo 8: Mapitio ya utekelezaji wa utaratibu katika usimamizi wa mabadiliko kwenye mifumo ya TEHAMA





Ukaguzi ulibaini changamoto katika usimamizi wa mabadiliko kwenye mifumo ya TEHA kwenye taasisi za umma zilizokaguliwa kama ifuatavyo:

(i) Kutokuwepo kwa taratibu za usimamizi wa mabadiliko kwenye mifumo ya TEHAMA

Kati ya taasisi 22 zilizokaguliwa, nne hazikuwa na taratibu za usimamizi wa mabadiliko kwenye mifumo ya TEHAMA, hivyo kuhatarisha usalama wa mifumo pale mabadiliko yanapotokea kama kufanyika kwa mabadiliko yasiyoidhinishwa. Kutekeleza taratibu ni muhimu kwa kupunguza hatari hizi na kuhakikisha mazingira salama kwa marekebisho ya mfumo.

(ii) Kutotenganisha mazingira ya majaribio na ya uzalishaji wa mifumo

Moja kati ya taasisi 22 haikuwa imetenganisha mazingira ya kujenga, kufanya majaribio, na uzalishaji wa mifumo ya TEHAMA, hivyo kuweka hatari kwa usalama wa mifumo. Mapungufu haya yanaweza kusababisha hitilafu isiyotarajiwa kwenye mifumo wakati wa majaribio na kuongeza uwezekano wa kukosa huduma zinazoratibiwa na mifumo hiyo. Pia inaweza kusababisha uharibifu wa data, na utumiaji wa mfumo usiohalali. Kukabiliana na changamoto hizi, taasisi zinashauriwa kutenga mazingira ya kujenga, kufanya majaribio, na uzalishaji kwenye mifumo ili kuhakikisha uadilifu katika mifumo.

(iii) Kutofanya majaribio ya usalama kabla ya kutekeleza mabadiliko

Taasisi saba kati ya 22 hazikuwa zimefanya majaribio ya usalama kabla ya kufanya mabadiliko na hivyo kuongeza hatari ya uwezekano wa udhaifu katika mifumo yao. Hii huzifanya taasisi kuwa kwenye hatari ya usalama unaoweza kuathiri uadilifu wa mifumo yake. Ni muhimu kwa taasisi kutekeleza taratibu za upimaji wa usalama ili kutambua na kushughulikia hatari kabla ya kutekeleza mabadiliko yoyote kwenye mifumo yao.

(iv) Kutofanya mapitio kwenye mifumo baada ya utekelezaji wa madadiliko

Nilibaini kuwa taasisi tisa kati ya 22 hazikuwa zimefanya mapitio baada ya kufanya mabadiliko kwenye mifumo ya TEHAMA. Kutofanya mapitio ya ufanisi na athari za mabadiliko kwenye mifumo kunazuia kujua tathmini ya ufanisi wa mabadiliko yaliyofanyika. Pia, inaweza pelekea kuwepo kwa masuala ambayo hayajapatiwa ufumbuzi, na kuongezeka kwa hatari za mifumo kukosa ufanisi kama ilivyokusudiwa. Taasisi hizi zinapaswa kulipa kipaumbele suala la mapitio




baada ya utekelezaji wa mabadiliko ili kurekebisha changamoto zinazoweza kujitokeza na kuongeza ufanisi wa mabadiliko kwenye mifumo husika ili kuendana na malengo na viwango vya taasisi hizi.

2.2.8 Usimamizi wa haki za utumiaji na ruhusa zinazotolewa kwa watumiaji wa mifumo - (ICT Systems Access Management)

Usimamizi wa upatikanaji wa haki za utumiaji na ruhusa kwa watumiaji wa mifumo unahusisha kudhibiti na kufuatilia ufikiaji halali wa watumiaji kwenye mifumo ya TEHAMA kwa kutumia sera, taratibu, mbinu, na zana mbalimbali ili kudumisha usalama wa mifumo na taarifa. Lengo la ukaguzi wangu lilikuwa kuthibitisha uwepo na utekelezaji wa taratibu zinazohusiana na ugawaji, uidhinishaji, na uondoaji wa uwezo wa kuingia kwenye mifumo kwa watumiaji. Pia ilijumuisha ukaguzi juu ya haki za uingiaji katika mifumo na shughuli zinazofanywa na watumiaji wa mifumo.

Nilifanya ukaguzi katika taasisi 22 za serikali ili kuhakikisha kama zinafuata taratibu zilizowekwa na serikali mtandaoni juu ya usimamizi wa haki za utumiaji na ruhusa zinazotolewa kwa watumiaji wa mifumo. Kiwango cha jumla cha taasisi hizi katika kufuata taratibu (compliance level) kimeoneshwa katika **Kielelezo Na. 9.**

Kielelezo 9: Tathmini ya ufuataji na uzingatiaji wa taratibu katika usimamizi wa haki za utumiaji na ruhusa zinazotolewa kwa watumiaji wa mifumo.



Matatizo yaliyobainishwa wakati wa ukaguzi wa usimamizi wa upatikanaji wa ruhusa za utumiaji wa Mifumo ya TEHAMA ni pamoja na yafuatayo:

(i) Kukosekana kwa taratibu za ugawaji na uondoaji wa haki za utumiaji wa mifumo

Ukaguzi wangu ulibainisha kuwa miongoni mwa taasisi 22 zilizokaguliwa, 14 hazina taratibu zilizoandikwa rasmi za kuwapatia na kuwaondolea haki za utumiaji wa mifumo kwa watumiaji jambo linalosababisha matumizi yasiyokuwa na idhini, kinyume cha miongozo ya serikali mtandaoni. Ili kulinda usiri wa data na kudumisha uadilifu wa mifumo ya taarifa, taasisi zinapaswa kuwa na sera na taratibu zilizoandikwa rasmi zinazoongoza ugawaji na uondoaji wa haki za utumiaji wa mifumo.




(ii) Kutofanya mapitio juu ya haki za watumiaji wa mifumo ya TEHAMA na shughuli zao

Wakati wa ukaguzi wangu, niligundua kuwa taasisi 13 hazikufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa shughuli za watumiaji na ruhusa za matumizi ya mifumo ya TEHAMA. Hii inaonesha kukosekana usalama wa taarifa ndani ya mifumo, hasa zile zinazohusiana na uingiaji kwenye mfumo usioidhinishwa, ambapo unauwezo wa kuingia bila kubainika. Ili kutatua tatizo hili, taasisi zinapaswa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara juu ya haki za ufikiaji wa watumiaji na shughuli za watumiaji.

2.2.9 Udhibiti wa mazingira ya miundombinu ya TEHAMA

Udhibiti wa mazingira ya miundombinu ya TEHAMA ni muhimu kwa kulinda usalama na uadilifu wa mifumo ya TEHAMA. Unashughulikia hatua mbalimbali kama vile usimamizi wa ufikiaji wa kwenye vituo vya data, udhibiti wa joto na unyevu, na ulinzi dhidi ya majanga ya asili na yaliyotengenezwa. Kutozingatia hatua hizi kunaweza kusababisha uharibifu wa vifaa vya TEHAMA, kupoteza data, na kukwamisha huduma. Katika ukaguzi wa mwaka huu, nilifanya tathmini katika taasisi za umma juu ya udhibiti wa ufikiaji katika vituo vya data, ikiwa ni pamoja na usimamizi wa ufikiaji wa milango, uwepo wa kamera za CCTV, na taratibu za matengenezo ya vifaa vya TEHAMA.

Nilifanya ukaguzi katika taasisi 22 za serikali ili kuhakikisha kama zinafuata taratibu zilizowekwa na serikali mtandaoni juu ya usimamizi wa mazingira ya miundombinu ya TEHAMA. Kiwango cha jumla cha taasisi hizi katika kufuata taratibu (*compliance level*) kimeoneshwa katika **Kielelezo Na. 10**.

Kielelezo 10: Tathmini ya udhibiti wa mazingira ya miundombinu ya TEHAMA.

Matatizo yaliyobainishwa wakati wa ukaguzi wa udhibiti mazingira ya miundombinu ya TEHAMA ni pamoja na yafuatayo:

(i) Ukosefu wa ufanisi katika udhibiti wa ufikiaji kwenye miundombinu ya TEHAMA

Nilibaini kuwa taasisi nne kati ya 22 hazina udhibiti wenye ufanisi katika ufikiaji katika mazingira ya miundombinu ya TEHAMA, hii ikiwa ni pamoja na kutokuwa na udhibiti wa ufikiaji wa milango na ukosefu wa daftari la wageni wanaozuru chumba cha Mitambo ya TEHAMA (server room). Hii inaruhusu kwa asiyehusika kuingia katika mfumo pasipo idhini, pia ni vigumu kufuatilia wageni hao ndani ya mfumo. Kupunguza hatari hizi kunahitaji utekelezaji udhibiti mkali wa ufikiaji katika mazingira yanayozunguka Miundombinu ya TEHAMA.

(ii) Kukosekana kwa kamera za usalama katika chumba cha Mitambo ya TEHAMA

Niligundua kuwa taasisi mbili kati ya 22 zilizokaguliwa hazina kamera za usalama katika vituo vyao vya data, na hivyo kusababisha changamoto katika kufuatilia sehemu hizo. Ili kuboresha usalama wa vituo vya data na uwezo wa kufuatilia shughuli, ni muhimu kwa taasisi hizi kufunga kamera za usalama.




2.2.10 Ununuzi na uundaji wa mifumo ya TEHAMA

Kupata mfumo mpya wa TEHAMA kwa taasisi za serikali kunahitaji kutambua mahitaji, ubunifu, na kutengeneza. Hii inaweza kufanywa na taasisi yenyewe au kwa kuajiri kampuni ya nje. Kufuata kanuni (viwango) zilizowekwa ni muhimu wakati wa kuunda mifumo hii.

Ukaguzi wangu ulilenga kuhakikisha kama mambo kadhaa muhimu yalifanyika kwa usahihi:

- kuweka kumbukumbu za watumiaji kwamba nini wanahitaji kutoka kwenye mfumo
- Kufuata sheria za uundaji wa programu (coding rules)
- Kufanya majaribio kamili ya mfumo
- Kupanga na kutathmini usalama wa mfumo
- Kuwa na mpango wa kuzindua mfumo, ikiwa ni pamoja na kuhama kutoka kwa mifumo ya zamani
- Kuwa na mpango wa ziada ikiwa kuna matatizo (mpango wa kurudi nyuma)
- Kuwafundisha watumiaji kuhusu mfumo mpya
- Kufuatilia kwa ukaribu jinsi mfumo unavyofanya kazi
- Kusimamia na kufuatilia kazi inayofanywa na kampuni zozote za nje zinazohusika katika maendeleo

Ukaguzi wangu uliangalia iwapo taasisi 22 za serikali zilifuata sheria zilizowekwa (viwango na miongozo ya mamlaka ya serikali mtandaoni) wakati wa kununua na kuunda mifumo mipya ya TEHAMA. **Kielelezo Na. 11** kinaonesha jinsi taasisi zilivyofuata sheria hizo.

Kielelezo 11: Tathimini ya manunuzi na uundaji wa mifumo ya TEHAMA

Wakati wa ukaguzi wa michakato ya manunuzi na uundaji wa mifumo ya TEHAMA, nilibaini masuala muhimu ya kuzingatiwa. Mambo muhimu yafuatayo yalipewa kipaumbele:

(i) Mapungufu kwenye nyaraka za mahitaji ya watumiaji wa mifumo ya TEHAMA

Taasisi moja ya serikali ilitengeneza mifumo mitano mipya, lakini sikuweza kupata uthibitisho wowote kwamba watumiaji wa mifumo hiyo walipitia na kuidhinisha mahitaji ya mifumo hiyo. Hii inaleta mashaka juu ya ubora wa mifumo hiyo au kutokidhi mahitaji halisi ya taasisi. Taasisi hizo zinapaswa kutoa kipaumbele uundaji wa nyaraka za mahitaji ya mfumo na kuhakikisha zinapitiwa na watumiaji kabla ya utekelezaji.

(ii) Kutofanyika jaribio la kukubaliwa Mfumo kwa Watumiaji.

Taasisi sita za serikali hazikufanya majaribio ya kukubaliwa mifumo mipya na Wadau ambao ndiyo watumiaji wa mifumo hiyo. Hii inaleta mashaka kwamba mifumo hiyo huenda haina ufanisi katika ufanyaji kazi, pia isiwe niyenye kutegemewa, au kukidhi mahitaji halisi ya watumiaji katika shughuli za kila siku. Taasisi za serikali zinahitajika kuhakikisha kwamba majaribio ya kukubaliwa mifumo yanafanywa na watumiaji wa mifumo hiyo kabla haijaanza kutumika.



(iii) Kutokufanya mapitio ya vyanzo vya misimbo(source codes)

Taasisi nne za serikali ziliacha hatua muhimu (mapitio ya vyanzo vya msimbo)) wakati wa mchakato wa kutengeneza mifumo mipya ya TEHAMA. Hii inamaanisha hakuna mtu mwingine aliyechunguza msimbo unaofanya kazi kwenye mifumo, ambayo inaweza kusababisha matatizo kama vile:

- Udhaifu wa usalama: Msimbo unaweza kuwa na udhaifu ambapo wadukuzi wanaweza kutumia.
- Makosa na hitilafu: Mifumo inaweza kutofanya kazi kama ilivyotarajiwa.
- Uwiano mdogo wa ubora: Msimbo unaweza kuwa dhaifu na kufanya mifumo iwe ngumu kudumisha au kusasisha baadaye.


Kutoizingatia hatua hii huongeza hatari na kupelekea mifumo kutoaminika au kutofaa kwa matumizi yanayokusudiwa. Taasisi za serikali zinapaswa kuhakikisha ukaguzi wa msimbo chanzo unafanywa wakati wa mchakato wa kutengeneza mfumo mpya.

2.2.11 Usalama wa taarifa

Ulinzi wa siri za taarifa za serikali (*usalama wa taarifa*) ni muhimu kuzuia upatikanaji usioidhinishwa na kuhakikisha taarifa zinabaki sahihi na zinapatikana. Kutokuwa na ulinzi imara wa taarifa unaongeza athari za mashambulizi ya kimtandao na uvujaji wa taarifa. Katika ukaguzi wangu, nilifanya tathmini katika vipengele kadhaa:

- Je, taasisi ina afisa maalum wa usalama wa taarifa?
- Je, taasisi hufanya tathmini za mapungufu na majaribio ya kuingia kwenye mifumo ya TEHMA ili kutambua udhaifu katika mifumo yao?
- Je, taasisi hutoa mafunzo ya uelewa wa usalama wa taarifa kwa wafanyakazi?

Ukaguzi huu uliangalia kama taasisi 22 za serikali zilifuata sheria zilizowekwa za usalama wa taarifa (viwango na miongozo ya serikali mtandaoni). **Kielelezo Na. 12** kinaonesha ni kwa namna gani taasisi za serikali zinafuata miongozo hiyo ili kuweka usalama wa taarifa kwenye mifumo ya TEHAMA.

Kielelezo 12: Mapitio ya Utekelezaji wa utaratibu katika usalama wa taarifa

Mapungufu yafuatayo yalibainishwa katika ukaguzi wa usalama wa taarifa:

(i) Kukosekana kwa afisa usalama wa taarifa za TEHAMA

Katika ukaguzi, nilibaini kuwa taasisi nne kati ya 22 hazikuwa na afisa usalama wa taarifa za TEHAMA. Kutokuwepo kwa mtaalamu huyo kunasababisha kukosekana kwa uangalizi katika kutekeleza na kufuatilia usalama wa taarifa, kufanya tathmini za viatarishi, na kushughulikia vikwazo vya usalama. Upungufu huu unaweka changamoto ya uwezo wa taasisi kutekeleza njia yenye ufanisi katika usalama wa taarifa. Taasisi zinapaswa kuhakikisha uwepo wa maafisa usalama wa taarifa za TEHAMA.

(ii) Kutofanya tathmini ya mapungufu na majaribio ya kuingilia Mifumo ya TEHAMA

Taasisi tano kati ya 22 hazikuwa zimefanya ukaguzi kamili wa usalama (tathmini ya mapungufu na majaribio ya kuingilia kimtandao) kwenye mifumo yao, jambo linaloweza kuwaacha katika hatari ya mashambulizi ya kimtandao. Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa ajili ya kubaini madhaifu kwenye mifumo ni muhimu kwa usalama wa taarifa. Ili kugundua na kutatua mapungufu hayo kwa wakati, taasisi zinapaswa kufanya tathmini za usalama mara kwa mara.

(iii) Kutofanyika mafunzo ya uelewa wa usalama wa taarifa kwa wafanyakazi

Nilibaini kuwa taasisi 12 kati ya 22 hazikutoa mafunzo muhimu ya uelewa wa usalama wa taarifa, hivyo kuashiria uwezekano wa kuongezeka kwa hatari ya vitisho vya usalama wa taarifa. Kuttoa mafunzo hayo kwa wafanyakazi kuongeza hatari ya kuweza kutokea mashambulizi ya kimtandao. Taasisi zinapaswa kutoa mafunzo ya uelewa wa usalama wa mifumo ya TEHAMA ili kupunguza hatari zinazoweza kutokea



SURA YA TATU

MIFUMO YA UHASIBU

3.0 Utangulizi

Kwa mujibu wa Mwongozo wa Utaratibu wa Uhasibu wa Mwaka 2021 (Toleo la Pili) wa Wizara ya Fedha, mfumo wa uhasibu wa Serikali (Tanzania Bara) unahusu mfumo unaotekelezwa na kufuatwa na taasisi zote za Serikali katika kukusanya, kuainisha, kurekodi, kufanya majumuisho, kuwasiliana na kutafsiri taarifa za fedha. Mfumo huu unahusika katika kujumlisha na kuakisi kwa kina miamala na matukio mengine ya kiuchumi yanayohusisha upokeaji, matumizi, uhamisho, utumiaji na utoaji wa mali na madeni.

Katika ukaguzi wangu wa mifumo ya uhasibu, nilijikita zaidi katika kutathmini ufanisi wa udhibiti wa mifumo katika mfumo wa MUSE, Epicor unaotumiwa na MSD, Serenic Navigator unaotumiwa na REA, na Sage Pastel unaotumiwa na TSN, Advanced Financial System unaotumiwa na Ngorongoro, na mfumo wa ERMS unaotumiwa na eGA. Nilichunguza vipengele muhimu kama vile udhibiti na uthibitishaji wa taratibu, upatikanaji wa ripoti muhimu za biashara, na utekelezaji wa ugawaji wa majukumu. Katika ukaguzi wangu, nilibaini mapungufu yafuatayo:

3.1 Usanifu usiotosheleza wa muunganisho kati ya MUSE na mifumo ya mapato

Katika tathmini yangu ya MUSE na mifumo ya mapato ya serikalini, nilibaini kuwa muundo wa sasa hurekodi tu bili zilizolipwa kama zinavyopokelewa kutoka GePG. Muundo wa sasa wa muunganisho haurahisishi uchapishaji wa moja kwa moja kwa bili zisizolipwa kutoka kwenye mifumo ya ukusanyaji wa mapato (bili) kwenda katika mifumo ya uhasibu, ambayo ni muhimu kwa uhasibu sahihi wa mapato.

Ninahusisha suala hili na muundo usiotosheleza wa majumuisho, ambao haukuzingatia kurekodi bili ambazo hazijalipwa kutoka kwenye mifumo ya kukusanya mapato hadi mifumo inayolingana ya uhasibu.

Utegemezi huu wa uingizaji wa tarakimu kwa mikono ili kunasa jumla ya mapato katika MUSE huleta hatari kubwa ya makosa na kutofautiana. Hatari

inayotazamiwa inaziweka taasisi kwenye upotoshaji wa taarifa za kifedha na changamoto za uadilifu wa taarifa.

Napendekeza Wizara ya Fedha iboreshe muunganisho wa mifumo ya mapato ya taasisi na mfumo wa uhasibu (MUSE) ili kuwezesha ufuatiliaji bora wa mapato na kuimarisha usimamizi wa fedha kwa ujumla.

3.2 Udhhibiti mdogo wa mfumo katika kusimamia viwango vilivyotumika katika ubadilishaji wa fedha dhidi ya malipo ya wazabuni

Kifungu cha 10.12 cha Mwongozo wa Uhasibu wa Wizara ya Fedha na Mipango (MoFP) wa Mwaka 2021 (Toleo la Pili) kinahitaji kwamba fedha za kigeni zibadilishwe kulingana na viwango vya wakati husika vya ubadilishaji wa fedha.

Ukaguzi wa mfumo wa MUSE katika taasisi ya EPZA ulibaini tatizo katika kuhakikisha mfumo unatumia viwango sahihi vya ubadilishaji wa fedha kama vilivyowekwa kwenye mfumo, hii ilipelekea matumizi ya viwango tofauti kwa tarehe ileile kwenye shughuli na benki ileile wakati wa malipo kwa wazabuni. mangufu haya yanaweza kusababisha makosa katika taarifa za kifedha.

Ninapendekeza kwamba uongozi wa EPZA uanzishe utaratibu rasmi na mwongozo wa maandishi wa usimamizi wa viwango vya kubadilisha fedha. Hii inapaswa kujumuisha ukaguzi wa mara kwa mara na kuimarisha udhibiti katika mfumo.

3.3 Uwekaji nambari za mfuatano usio sahihi

Mfumo wa Serenic Navigator una hitilafu katika mtindo wa kuhesabu nambari. Hii ni kwa sababu ya dosari katika muundo wa Kikokotoo katika uchakataji (algorithm). Kulikuwa na mapungufu katika nambari za ankara. Hii inaweza kusababisha ugumu katika kufuatilia maagizo na upatanisho wa akaunti, ambayo inaweza kusababisha ripoti za kifedha zisizo sahihi.

Ninapendekeza kufanyike mapitio ya kina na uboreshaji wa kikokotoo (algorithm) ya mfuatano wa kutengeneza nambari za mkataba wa ununuzi na bili.

3.4 Kutolingana kati ya mkataba wa manunuzi na kiasi kilichohitajika

Mfumo wa Epicor katika MSD hauna udhibiti wa kutosha ili kulinganisha kiasi cha mkataba wa manunuzi dhidi ya mahitaji halisi. Hii imesababisha manunuzi ya vifaa 287 kuwa zaidi ya mahitaji halisi, na manunuzi ya vifaa 3,137 yanayofadhiliwa na MSD kutokuwa na mahitaji halisi. Hili linaweza likatoa fursa kwa shughuli za ubadhirifu, kama vile kuunda mikataba ya manunuzi ambayo haikuidhinishwa au kupandisha bei, na hivyo kusababisha hasara za kifedha.

Ninapendekeza menejimenti ya MSD: (a) Kutekeleza udhibiti wa mfumo ili kuhakikisha kwamba Mikataba ya manunuzi inalingana na Mahitaji halisi; na (b) Kuweka mipangilio ya mfumo ili kuzuia uundaji wa Mikataba yenye idadi inayozidi mahitaji halisi.

3.5 Mapokezi ya vifaa bila ya kuwa na mahitaji wala mkataba

Mfumo wa Epicor katika MSD hauna udhibiti wa kutosha wa kuzuia upokeaji wa bidhaa bila mahitaji halisi na mkataba wa manunuzi. Hii imejitokeza ambapo vifaa 37 vilipokelewa bila ya kuwa na ushahidi wa mkataba wa manunuzi wala mahitaji halisi, na vifaa 4 vilipokelewa vikiwa na ombi la ununuzi lakini havikupatikana katika mkataba wa manunuzi.

Suala hili linatokana na mapungufu ya muundo wa mfumo, kuruhusu mapokezi kushughulikiwa bila mahitaji yanayolingana na mkataba wa manunuzi.

Mapokezi ya bidhaa zisizolingana yanaweza kusababisha makosa ya hesabu na mchakato wa manunuzi, hii inaweza kusababisha kuongezeka au kupungua kwa akiba, hivyo kuathiri uendeshaji na bajeti. Rekodi zisizolingana ya Hati ya bidhaa zilizopokewa dhidi ya mkataba wa manunuzi na mahitaji halisi huhatarisha uadilifu wa taarifa.

Ninapendekeza menejimenti ya MSD kutekeleza udhibiti unaofaa kwenye mfumo unaozuia mabadiliko ya nambari ya bidhaa kwa wafanyikazi walioidhinishwa na kutekeleza udhibiti kati ya GRNs, POs, na rekodi za mahitaji ili kuhakikisha usahihi na uadilifu wa taarifa ya ununuzi.

3.6 Bili zilizotolewa bila hati ya vifaa vilivyopokelewa

Mfumo wa Epicor katika MSD ukiwa na udhibiti mdogo unaohakikisha bili (Invoice) zinatolewa kutoka kwenye Hati za bidhaa zilizopokelewa. Ukaguzi wangu umebaini kuwepo kwa bili za vifaa 148 vilivyotolewa bila taarifa ya mapokezi ya vifaa (GRN). Nambari ya kumbukumbu ya GRN iliyobainishwa, nambari ya mkataba wa manunuzi (PO), na nambari ya PO ya bili hizi hazikupatikana kwenye orodha ya GRN zote. Hii inasababishwa na udhibiti mdogo wa mfumo ili kutekeleza uundaji wa ankara za akaunti zinazolipwa kulingana na GRN.

Bila GRN ya kuthibitisha upokeaji wa vifaa au huduma, kuna hatari ya kwamba shirika linaweza kulipia vifaa ambavyo havikupokea.

Ninapendekeza menejimenti ya MSD iimarisha udhibiti wa IFMS Epicor ili kulinganisha bili na GRN ipasavyo ili kuhakikisha ankara zitolewe kulingana na GRN.

3.7 Kutokuwa na uwiano kati ya hati ya mapokezi ya vifaa na mkataba wa manunuzi

Ndani ya mfumo wa Epicor kuna udhibiti mdogo wa kulinganisha kati ya vifaa vilivyopokelewa dhidi ya kiasi kilichoagizwa kwa ajili ya manunuzi. Hii imedhihirika pale ambapo kiasi kilichopokelewa kilikuwa ni kikubwa zaidi ya kiasi kilichoagizwa., vile vile, kuna bidhaa zilizopokelewa ambazo zina kiasi kikubwa kuliko ilivyoagizwa. Hii inasababishwa na kutokuwa na udhibiti wa kutosha katika wa mfumo wa Epicor juu ya ulinganishaji kati ya wa GRN na PO.

Tofauti za idadi na kiasi kwenye GRN na PO zinaweza kusababisha hitilafu za kifedha, kuathiri usahihi wa taarifa za fedha na uwezekano wa kusababisha hasara za kifedha. Kupokea bidhaa kupita kiasi kunaweza sababisha kuwa na mlundikano wa bidhaa nyingi zisizokuwa na tija ambazo pia zitachangia kuwa na gharama kubwa zisizokuwa kwenye bajeti kwa ajili ya ubebaji na kuzihifadhi.

Ninapendekeza kwamba menejimenti ya MSD iimarishe udhibiti wa mfumo wa Epicor ili uweze kulinganisha kati ya GRN na PO ili kuzuia tofauti kati ya idadi ya bidhaa zilizounuliwa dhidi ya kiasi kilicholipwa.

3.8 Uingizaji wa malipo kwa njia ya mkono (Manual)

Katika ukaguzi wangu niliufanya juu ya malipo ya wazabuni katika Mfumo wa Kifedha (Advanced Financial System) unaotumiwa na Mamlaka ya hifadhi ya eneo la Ngorongoro, nilibaini kuwa mhasibu huingiza malipo hayo kwa njia ya mikono badala ya Mfumo wenyewe kuchukua moja kwa moja kiasi hiko kutoka kwenye LPO iliyopo ndani ya mfumo, hii inasababishwa na mapungufu ya mfumo kushindwa kuhusanisha nyaraka hizo moja kwa moja, hivyo hupelekea hatari ya kuingiza malipo yanayozidi thamani halisi ya LPO iliyo dhinishwa pia kuongeza hatari za hitilafu na kusababisha malipo yasiyo sahihi kwa Wazabuni.

Ninapendekeza kwamba menejimenti ya NCAA iimarishe ufanisi wa mfumo wa Kifedha ili ufanye kazi moja kwa moja ya kuweza kuhusanisha malipo kutoka kwenye LPO ndani ya mfumo dhidi ya Mzabuni husika anayelipwa ili kuepuka makosa ya kufanya malipo zaidi ya kiasi katika LPO.

3.9 Udhibiti usiotosheleza wa mfumo katika kusimamia masurufu ya watumishi

Uchunguzi wa usimamizi wa masurufu ya watumishi umebaini makosa yafuatayo:

- a) Mfumo wa ERMS unaotumiwa na eGA hauna udhibiti wa kutosha katika kuzuia utoaji wa masurufu kwa wafanyakazi ambao tayari wana masurufu ambayo hayakurejeshwa. Upungufu huu umesababisha kufanya malipo ya masurufu kwa watumishi ambao hawakurejesha masurufu ya awali.

- b) MUSE inaruhusu kuunda zaidi ya hati moja ya malipo kwa kutumia nyaraka moja ya masurufu na kusababisha malipo zaidi ya kiasi cha masurufu kilichoidhinishwa.

Makosa yaliyobainika yanasababishwa na muundo wa mifumo kutojitosheleza katika kuendana na masharti ya kisheria ambayo yanasisitiza urejeshaji wa masurufu kabla ya kutolewa kwa masurufu mapya.

Udhibiti usiojitosheleza wa mfumo katika kuzuia utoaji wa masurufu mapya kwa wafanyakazi kabla ya usuluhishi wa masurufu ambayo hakurejeshwa hudhoofisha udhibiti wa mfumo wa ndani unaohakikisha urejeshaji wa masurufu kwa wakati.

Ninapendekeza menejimenti ya Wizara ya Fedha na Mamlaka ya Serikali Mtandaoni kuimarisha udhibiti wa mifumo ili kuhakikisha masurufu yanatolewa kwa watumishi ambao hawana deni la masurufu ya awali, pia malipo yasizidi masurufu yaliyoidhinishwa.

3.10 Mgawanyo usiotosheleza wa majukumu katika hatua za malipo

Ukaguzi wangu ulibaini mapungufu katika namna Wizara ya Fedha (MoF) na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) zinavyosimamia taratibu zao za malipo. Hasa, ukaguzi ulibaini ukosefu wa mgawanyiko wa majukumu, ambayo ina maana kwamba baadhi ya watendaji wana lazimika kufanya hatua nyingi muhimu katika mchakato bila uangalizi mzuri ambao huongeza hatari ya makosa au udanganyifu. Masuala mengine yaliyopatikana yameorodheshwa hapa chini:

- Kulikua na matukio katika mfumo wa MUSE ambapo watendaji binafsi wanaweza kuunda na kuidhinisha Hati za malipo wenyewe.
- Matukio mawili katika MUSE ambapo watu binafsi wanaweza kuunda na kuidhinisha rekodi za washitiri wao wenyewe.
- Watumiaji wanaweza kubadilisha marekebisho ya hati za malipo pasipo ukaguzi katika Serenic Navigator.
- Manunuzi katika MUSE yalikosa mwidhinishaji aliyekabidhiwa.
- Wafanyakazi wanaotengeneza mkataba mdogo wa manunuzi katika mfumo wa Epicor unaotumika MSD hawakuwa na wasimamizi waliowekwa kwenye mfumo, hivyo kuwaruhusu kuruka hatua ya uidhinishwaji.
- Katika NCAA michakato muhimu ikijumuisha marekebisho ya bajeti, marekebisho ya idadi ya hesabu za mali, na ubadilishaji wa ununuzi/ankara ndani ya mfumo hauna hatua ya uidhinishaji.

Mapungufu yaliyobainika husababishwa na mchakato usiotosheleza wa kukusanya mahitaji wakati wa uundaji wa mifumo.

Ukosefu wa mgawanyo wa majukumu huongeza hatari ya udanganyifu au makosa kutokana na ukosefu wa uangalizi. Pia, inahatarisha uadilifu wa miamala na uwajibikaji.

Ninapendekeza kwamba menejimenti za Wizara ya Fedha, MSD, REA na NCAA uimarishe muundo wa udhibiti unaohakikisha kwamba hatua mbalimbali za malipo zinajumuisha mgawanyo wa majukumu.

3.11 Utoaji wa ripoti na taarifa za fedha zenye makosa

Mfumo wa ERMS unaotumiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandaoni hutoa ripoti zenye makosa kama ilivyoelezwa hapa chini:

- Tofauti zilipatikana katika jumla ya matumizi katika vifungu mahususi vya matumizi katika ripoti iliyobainishwa ikilinganishwa na matumizi halisi.
- Salio hasi la kuanzia na kufungia kwa bidhaa katika ripoti ya hesabu za mali

Hitilafu hii inatokana na uhakiki mdogo wa ripoti za mfumo unaofanywa na watumiaji. Hitilafu katika ripoti zinaweza kusababisha takwimu za kifedha zisizo sahihi na maamuzi ya uendeshaji kwa kutumia taarifa zisizo sahihi.

Ninapendekeza kwamba Mamlaka ya Serikali Mtandao (a) ikague ripoti zote katika sehemu ya ripoti ya ERMS kwa ushirikiano na idara za watumiaji, na (b) Ihakikishe usahihi wa uzalishaji wa taarifa kutoka katika kanzidata.

3.12 Uandaaji wa taarifa za kifedha nje ya mfumo

Taarifa muhimu za kifedha kama vile taarifa ya Mizania ya kifedha, taarifa jumuiifu ya mapato na matumizi, na taarifa za mtiririko wa fedha hazitolewi kiotomatiki na mfumo wa uhasibu wa Serenic Navigator unaotumiwa na REA.

Mapungufu yaliyobainika yalitokana na ukosefu wa mahitaji sahihi ya watumiaji wakati wa utengenezaji wa mfumo. Maandalizi ya taarifa za fedha nje ya mfumo huongeza hatari ya makosa na kupunguza ufanisi.

Ninapendekeza kwamba menejimenti REA (a) isisitize na kuweka kipaumbele kwa kutumia mfumo wa Serenic Navigator kwa kuandaa taarifa za fedha; na (b) Kufanya utafiti na kuja na njia bora za kuwezesha uundaji na utolewaji wa taarifa muhimu za kifedha kiotomatiki.

3.13 Changamoto za muunganiko kati ya mifumo ya MUSE na HCMIS

Kulikuwa na tofauti zilizopatikana katika mshahara na tozo za kisheria kati ya mfumo wa HCMIS na MUSE. Kutofautiana huku kulionesha hitilafu ambayo inasababisha taarifa za kifedha zisizo sahihi.

Napendekeza kwamba Wizara ya Fedha itekeleze maboresho ya ushirikiano wa taarifa ili kuhakikisha usahii wa taarifa za mishahara kati ya HCMIS na MUSE.

3.14 MUSE inaruhusu matumizi kupita kiasi zaidi ya Bajeti Iliyotengwa

Mfumo uliruhusu kuzidi kwa bajeti iliyoidhinishwa kwa sababu matumizi yaliyolipwa moja kwa moja na Wizara ya Fedha kwa niaba ya taasisi nyingine hayakuoneshwa moja kwa moja, hivyo kusababisha uwiano wa pesa zilizopo kuonekana kuwa kubwa zaidi kuliko ilivyo halisi, kuruhusu taasisi kutumia zaidi ya ile bajeti iliyopitishwa.

Pia, bajeti iliyotengwa kwa ajili ya mishahara iletwa kutumika katika matumizi ya ujenzi yasiyoruhusiwa, hivyo kuhatarisha usimamizi wa fedha na taratibu za kiuhasibu.

Ninapendekeza kwamba Wizara ya Fedha: (a) Kuboresha Mfumo wa Usimamizi wa Matumizi ya Serikali (MUSE) ili kutambua moja kwa moja malipo yote ya Wizara ya Fedha, kuzuia matumizi ya ziada; (b) iimarisheni uhibiti wa mfumo ili kuzuia uainishaji mbaya wa matumizi na kutekeleza mgawanyo sahihi wa bajeti.

3.15 Mapungufu katika uhasibu wa mishahara kivuli (Dummy Salary) katika MUSE

Gharama za mishahara “dummy salaries” ziliingizwa moja kwa moja kupitia dirisha la leja ya jumla “General Ledger”, kupelekea kukwepa uidhinishaji unaohitajika na uwezekano wa kuficha shughuli za ubadhirifu.

Pia, taarifa za mishahara “dummy salaries” kwa baadhi ya miezi haikuwekwa kwenye MUSE, na kusababisha taarifa za kifedha kupotoshwa. Hii ilitokana na utaratibu wa uingizaji wa taarifa za mishahara hiyo kwa mikono katika MUSE badala ya kuingiza kiotomatiki katika leja ya jumla baada ya malipo .

Ninapendekeza kwamba Wizara ya Fedha (a) kubuni upya dirisha la marekebisho katika MUSE ili kuzuia uchapishaji usioidhinishwa wa gharama za mishahara; na (b) kuhakikisha uingizwaji wa gharama za mishahara kiotomatiki katika leja ya jumla ya mfumo wa MUSE ili kuhakikisha ripoti sahihi ya kifedha.

3.16 Matumizi yasiyofaa ya mifumo

Ukaguzi wangu ulibainisha matukio kadhaa ya matumizi yasiyofaa ya mifumo katika mashirika mbalimbali ya serikali, jambo lililoibua mashaka kuhusu uwazi wa masuala ya kifedha, uwajibikaji na misingi ya uadilifu.

a) Wizara ya Fedha

- **Kukwepa mikataba ya manunuzi** : Malipo yaliyoingizwa kwenye leja ya jumla ya mfumo bila mikataba ya manunuzi.

Ninapendekeza kwamba Wizara ya Fedha itekeleze udhibiti ili kuzuia kutumia dirisha la kawaida la hati za malipo yanayohitaji mikataba ya manunuzi;

b) Wizara ya Mifugo na Uvuvi - Sekta ya Uvuvi

- **Utolewaji wa bili za mapato kwa njia ya kawaida (mikono):** Bili zinazohusiana na mfumo zikiwa na jumla ya zaidi ya bilioni 1.4 zilitolewa kwa njia ya mikono kupitia moduli ya "bili nyinginezo", hivyo kuibua mashaka kuhusu ufanisi na uwezekano wa matumizi mabaya.
- **Ukosefu wa ufuatiliaji wa vibali:** Vibali na leseni zinazolipiwa kupitia kifungu cha "mengineyo" hazikufuatiliwa ndani ya mfumo, na hivyo kuibua mashaka jua ya utii wa sheria na usahihi wa taarifa.

Ninapendekeza kwamba Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi) kuzuia matumizi ya moduli "bili nyinginezo" kwa njia ya kawaida bali yafanywe kupitia bili za kiotomatiki na kufuatilia matumizi ya mfumo kwa kuzingatia utii wa sheria.

c) Mamlaka Ya Dawa Na Vifaa Tiba (TMDA)

Uzalishaji wa Bili nje ya mfumo rasmi: Bili zinazofaa kuandaliwa kwa mfumo ziliundwa katika sehemu isiyo ya rasmi, kukosa idhini zinazofaa na uwezekano wa kusababisha upotevu wa mapato.

Ninapendekeza kwamba TMDA iimarisha usimamizi ili kuhakikisha matumizi sahihi ya mfumo na kufuata taratibu zilizowekwa.

3.17 Kuchelewa kuchapisha miamala katika mfumo wa MUSE

Ukaguzi wangu ulibaini mapungufu katika MUSE yalikuwa yakihusiana na ucheleweshaji wa uchapishaji wa miamala. Mfumo uliruhusu miamala 827 kutumwa baada ya tarehe ya mwisho iliyowekwa ya tarehe 15 ya mwezi

unaofuata, kuanzia siku 3 hadi miezi 4 kuchelewa. Machapisho haya yaliochelewa yalikosa ushahidi wa kibali sahihi.

mapungufu haya yalitokana na udhibiti mdogo wa mfumo katika kuthibitisha tarehe ya uchapishaji.

Tofauti iliyobainika iliathiri kutoaminiwa taarifa ya fedha kwa sababu ya kutokuamikina kwa data katika Leja Kuu (General Ledger).

Ninapendekeza kwamba Wizara ya Fedha iimarise udhibiti wa mfumo kwa kutekeleza ukaguzi wa uthibitishaji ili kutekeleza tarehe ya mwisho ya uchapishaji wa miamala ya tarehe 15 ya mwezi unaofuata.

3.18 Uingiaji pamoja na matumizi yasiyoidhinishwa katika mfumo wa Fedha

Ukaguzi wangu umebaini kuwepo kwa ukiukwaji wa usalama katika mfumo wa kiuhasibu wa REA ambapo mtu asiye stahili alipata uwezo wa kutumia mfumo katika kuunda ankara na hati za malipo. Mtu huyu ambaye si Mtaalamu sahihi wa uhasibu, pia miamala aliyofanya ilkwepa taratibu za uidhinishaji zilizowekwa.

Changamoto iliyobainika ilitokana na udhibiti mdogo wa utoaj wa hak za kutumia mfumo na usimamizi mdogo juu ya jukumu la mtumiaji.

Hii ina athari kwa kuongezeka kwa hatari ya ubadhirifu. Pia, kuna uwezekano wa kutokuwa sahihi kwa rekodi za kifedha kutokana na ukosefu wa ujuzi wa mtumiaji.

Ninapendekeza kwamba menejimenti ya REA (a) kuhakikisha watumiaji wanakuwa na kiwango cha chini cha matumizi ya mfumo kinachohitajika kwa majukumu yao ya kazi; (b) kuhakikisha wafanyakazi wanaelewa majukumu na wajibu wao, ikijumuisha taratibu zinazofaa za kushughulikia taarifa; na (c) Kutenganisha majukumu ya kuanzisha, kuidhinisha na kurekodi miamala ili kupunguza hatari ya shughuli zisizoidhinishwa.

3.19 Uhamishaji wa fedha za bakaa kwa njia ya kawaida katika mfumo wa MUSE

Benki Kuu ya Tanzania (BOT) wana mfumo ambao huhamisha fedha za bakaa moja kwa moja kutoka Akaunti Moja ya Hazina (Treasury Single Account) kwenda kwenye akaunti ya mtiririko wa fedha (Cash Flow Account) mwishoni mwa mwaka wa fedha (Juni 30).

Hata hivyo, MUSE inahitaji uingizaji wa taarifa kwa njia ya kawaida (manual) ili kuonesha uhamisho huu katika Kitabu cha Pesa cha TSA.

Athari za uingizaji huu wa taarifa ni kwamba: (a) inatumia ongezeko la muda na nguvu; (b) ni rahisi kuwa na makosa, ambapo inaweza kuathiri usahihi wa rekodi za kifedha; na (c) Kutowiana kati ya mifumo kunaweza kuibua mashaka kuhusu kutegemewa kwa taarifa ya kifedha.

Ninapendekeza kwamba menejimenti ya Wizara ya Fedha inapaswa kuweka kipaumbele katika uimarishaji wa mfumo wa MUSE ili kuharakisha uhamishaji wa fedha za bakaa, na kuondoa hitaji la kuingiza taarifa kwa mikono.

3.20 Kutokuwepo kwa uhamishaji wa taarifa za mifumo katika Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)

Ukaguzi wangu umebaini kuwa TMA haijahamisha takwimu kutoka kwenye mfumo wao wa zamani wa hesabu (Epicor) kwenda kwenye Mfumo mpya wa Malipo wa Serikali (MUSE). Hii ni kutokana na kutokuwepo kwa mpango rasmi wa uhamishaji taarifa.

Kukosekana kwa taarifa iliyohamishwa kutoka mfumo wa awali kunaweza sababisha taarifa zisizo sahihi za kifedha katika mfumo mpya.

Ninapendekeza kwamba Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA): (a) iandae mchakato wa kuhamisha taarifa kutoka Epicor hadi MUSE, ili kuhakikisha uzingatiaji wa miongozo ya Serikali Mtandaoni; na (b) kutekeleza mpango wa kuhamisha taarifa muhimu kutoka kwenye mfumo wa zamani hadi mpya.

SURA YA NNE

MAPATO

MIFUMO YA MAPATO

4.0 Utangulizi

Sura hii inabainisha umuhimu wa kuboresha mifumo ya ukusanyaji mapato ya serikali ya Tanzania. Inazingatia mapungufu yaliyo onekana katika idara mbalimbali, ikiwa ni pamoja na ada ambazo hazikujumuishwa katika mchakato wa bili na udhibiti usiojitosheleza katika kuzuia malipo ya mteja ya huduma moja kutumika kulipa ada za huduma zilizo ongezeka. Mapungufu haya yanachangia hasara, ufanisi mdogo katika utendaji kazi, na uwezekano wa kutozingatia kanuni. Ripoti hii inatoa mapendekezo mahususi kwa kila idara kushughulikia masuala haya muhimu.

4.1 Vibali vya usafirishaji wa samaki nje ya nchi vilivyotolewa bila malipo

Ukaguzi wa mfumo wa FiRCIS ulio chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ulibaini kua kibali cha Usafirishaji wa Samaki nje ya nchi (EP2229000108) kilikabidhiwa bila malipo yanayopaswa kulipwa kabla ya utoaji wa kibali. Hii ilichangiwa na mapungufu katika mfumo. Tukio hili linaonyesha uwezekano wa kupoteza mapato zadi ikiwa udhibiti katika mfumo hautoboreshwa ili kuhakikisha malipo yanakusanywa kabla ya vibali kutolewa.

Kutoa vibali vya Usafirishaji wa Samaki nje ya nchi kwa wateja kabla ya kupokea malipo kunapelekea hasara ya mapato kwa serikali.

Napendekeza uongozi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (sekta ya uvuvi) kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kutambua na kushughulikia hitilafu za kiufundi, na makosa ya mfumo huku wakihakikisha mafunzo kwa wafanyakazi ili kudumisha usalama wa mfumo.

4.2 Wanafunzi waliodahiliwa bila ada ya maombi

Katika Mfumo wa Maombi Mtandaoni (OAS) unaotumiwa na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) kulikuwa na kumbukumbu za waombaji 50 zenye jumla ya ada ya shilingi 500,000 ambazo zilikuwa na namba za udhibiti zilizorudiwa (bili). Hii

inamaanisha kwamba, malipo kwa namba moja ya udhibiti yanaweza kutumika kulipia ada ya maombi ya mwombaji mwingine.

Hivyo hivyo, katika mfumo wa SARIS unaotumiwa na Chuo Kikuu Huria kulikuwa na kumbukumbu za wanafunzi 40 zenye jumla ya ada ya mtihani ya shilingi 1,670,000 na kumbukumbu za wanafunzi 71 zenye jumla ya ada ya karo ya shilingi 20,455,500, ambazo zilikuwa na namba za risiti za malipo zilizorudiwa.

Hali hii inasababishwa na udhibiti mdogo wa uthibitisho katika mfumo wa SARIS; na mifumo ya Udahili Mtandaoni inayoruhusu kurudiwa kwa namba za udhibiti na risiti za malipo, pamoja na ukosefu wa mawasiliano kati ya GePG na SARIS.

Ninapendekeza uongozi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (a) kuboresha udhibiti wa uthibitisho wa malipo katika mifumo yake ya bili ili kuzuia kurudiwa kwa namba za udhibiti na risiti; na (b) kufuatilia upungufu wa malipo ulioainishwa ili kuhakikisha kuwa malipo yanayohitajika yanatatuliwa ipasavyo.

4.3 Uzalishaji wa risiti nyingi kwa malipo yaliyofanyika mara moja

Katika Sage Pastel inayotumiwa na TSN, mfumo unaruhusu malipo yaliyofanyika mara moja kutumika kuzalisha risiti nyingi na kulipia ankara mbalimbali za wateja zisizohusiana kimakosa kuonesha kwamba zimelipwa.

Mapungufu haya yanatokana na kasoro ya usanifu na utekelezaji wa mfumo ambao hauzui malipo ya kitu kimoja kutumika kinyume kulipia huduma nyingine

Ninapendekeza uongozi wa TSN kuboresha mfumo ili uwe na uwezo wa kuthibitisha malipo ambayo itaboresha uwezo wa mfumo kuzuia shughuli za udanganyifu wa malipo.

4.4 Mfumo kutoweza kukokotoa marekebisho ya tozo za VISA kielektroniki

Mfumo wa idara ya uhamiaji (e-services) hauna uwezo wa kukokotoa tozo. Mhasibu anahitajika kukokotoa kwa mikono na kuingiza kwenye mfumo, hii hupelekea makosa.

Hili lilisababishwa na muundo wa mfumo kutojitosheleza katika kujumuisha vipengele vya kuchakata maelezo ya mtu yanayohusu VISA.

Suala la Mhasibu kukokotoa na kuingiza kiasi cha bili kwa mkono, huweka uwezekano wa makosa ya kihesabu, na kuleta hatari ya kutokuwa na uadilifu katika mchakato wa marekebisho ya bili.

Ninapendekeza uongozi wa Uhamiaji kuboresha mfumo ili uwe na uwezo wa kukokotoa kiasi cha ongezeko la ada pindi itokeapo marekebisho.

4.5 Malipo yaliyojirudia katika mfumo wa RRIMS

Mfumo wa RRIMS unaotumiwa na LATRA unarekodi muamala mmoja mara nyingi, hali inayopelekea uwepo wa taarifa za mapato zisizo sahihi.

Hii inasababishwa na mapungufu katika muundo wa mfumo, unaruhusu miamala ya bili kujirudia.

Kurekodi miamala maradufu kunaweza kupelekea malipo ya bili zisizo sahihi, na makosa katika uandaaji wa taarifa za fedha.

Ninapendekeza uongozi wa LATRA uboresha mfumo wa RRIMS ili kuzuia makosa katika kujirudia kwa miamala; pia wafanye ukaguzi na ufuatiliaji mara kwa mara kuhakikisha kwamba mapungufu kama haya hayajitokezi tena siku za usoni.

4.6 Faini ambazo hazikulipwa katika mfumo wa RRIMS

Kulikuwa na makosa 32 kwa ajili ya faini katika mwaka wa fedha 2022/23 ambapo kiasi kilicholipwa kilikuwa chini ya kiasi kilichotozwa, ikimaanisha kuna faini ambazo hazikulipwa na kupelekea upotevu wa mapato ya serikali. Mapungufu haya yanatokana na udhibiti mdogo kuhakikisha kiwango kilichotozwa kinaendana na kiwango kilicholipwa.

Ninapendekeza uongozi wa LATRA uboresha mfumo wa RRIMS kwa kutekeleza udhibiti unaohakikisha kiasi kilicholipwa kinaendana kikamilifu na kiasi kilichotozwa.

4.7 Mpungufu katika makusanyo ya nje ya mtandao wa TAUSI MIS

Mfumo wa TAUSI hauna udhibiti juu ya makusanyo ya nje ya mtandao kupitia vifaa vya POS. Hakuna kiasi kilichowekwa kwa ajili ya makusanyo nje ya mtandao, hii hupelekea mianya ya makusanyo mengi ya mapato kufanyika nje ya mtandao kwa muda mrefu.

Mapungufu haya yanatokana na kutoweka kiwango au kiasi kinachoruhusiwa kukusanywa nje ya mtandao na kutoweka muda ambao afisa anaruhusiwa kukusanya akiwa nje ya mtandao.

Ninapendekeza TAMISEMI itoe muongozo utakaoelekeza kiwango kinachotokana na makusanyo nje ya mtandao kwa kila wakala.

4.8 Mfumo wa TAUSI kushindwa kutoa bili kiotomatiki

TAUSI haiwezi kutoa bili kiotomatiki. Bili zinatengenezwa na wakusanyaji au wahasibu wa mapato, hii inapelekea ucheleweshwaji katika kutengeneza bili.

Changamoto hizi zinatokana na mapungufu katika muundo wa mfumo.

Ninapendekeza uongozi wa TAMISEMI kuwezesha mfumo kutengeneza bili kiotomatiki.

4.9 Changamoto ya mifumo ya kutengeneza bili katika kuwasiliana na mfumo wa GePG

Mifumo ya bili ya RIMS ya TMDA na TOS ya TPA haina udhibiti wa kuhakikisha miamala inayofanyika katika mifumo yao inafika GePG. Hii ilipelekea ankara 20 zilizositishwa (cancelled) kutoka RIMS na 132 kutoka TOS kutositishwa katika mfumo GePG. Hivyo ikapelekea malipo ya ankara zilizositishwa.

Changamoto hii inaweza kupelekea tofauti za kifedha zilizo ripotiwa kati ya mifumo ya bili na MUSE.

Ninapendekeza uongozi wa TMDA na TPA warekebishe mifumo yao kwa ushirikiano na uongozi wa GePG ili kuhakikisha miamala inayositishwa katika mifumo yao iweze kusitisha pia katika mfumo wa GePG .

4.10 Usajili wa bidhaa na mchakato wa kutoa Bili wenye kasoro kutokana na uingizaji kutumia Mkono

Katika mchakato wa kutengeneza bili za usajili wa bidhaa ,afisa anatakiwa kuchagua kundi la gharama ambapo hii huongeza hatari ya kufanya makosa kwa kuchagua kundi lisilo sahihi.

Chanzo cha mapungufu haya inatokana katika uandaaji na utekelezaji wa mahitaji ya mfumo.

Ninapendekeza uongozi wa TMDA uboreshe mfumo ili uweze kutambua kundi la gharama pasipo kuhitaji uingizaji kwa mkono.

4.11 Mfumo wa TAUSI hauwezi kuzuia ukusanyaji katika POS zaidi ya kiwango kilichowekwa

Mfumo wa TAUSI MIS haudhibiti vifaa vya POS ipasavyo, hivyo kupelekea kuruhusu kufanya miamala yenye thamani zaidi ya kiwango kilichowekwa kwenye kifaa hiko. Hii imepelekea vifaa 114 vya POS kufanya miamala inayozidi viwango vya pesa vilivyowekwa kwenye vifaa husika, kinyume na inavyopaswa ambapo miamala inapaswa kupunguzwa kutoka kwenye kiwango kilichotengwa. Dosari hii inatokana na upungufu katika muundo wa mfumo, unaofanya mfumo usiweze kudhibiti makusanyo katika kifaa cha POS dhidi ya kiwango kilichowekwa kwa ufanisi.

Udhaifu huu unaathiri uratibu wa fedha, na kufanya iwe vigumu kufuatilia na kusimamia fedha zilizokusanywa kupitia vifaa vya POS.

Napendekeza kwamba manajimenti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI (a) itathmini na kufuatilia vifaa vya POS ambavyo vimerekodi miamala zaidi ya viwango vyao; na (b) kuboresha mfumo ili kuhakikisha kwamba POS haiwezi kufanya miamala zaidi ya kiwango kilichotengwa.

4.12 Ada za Maji Taka zisizo sahihi katika MAJI IS

MAJI IS huko MWAUWASA unakosa udhibiti wa kuthibitisha ada zilizowekwa dhidi ya ada zilizoidhinishwa. Hii imepelekea kuingizwa kwa ada za maji taka zisizo sahihi kwa wateja wa majumbani.

Hii ni kutokana na kukosekana kwa mapitio na uthibitishaji wakutosheleza katika mfumo.

Ada za maji taka zisizo sahihi katika mfumo zinasababisha kupotea kwa mapato na kuwatoza wateja wa makazi zaidi.

Ninapendekeza kwamba menejimenti ya MWAUWASA (a) ipitie ada zote zilizoingizwa katika MAJI IS na kuhakikisha zinaendana na ada zilizoidhinishwa; na (b) Uanzishwe utaratibu wa usimamizi wa mabadiliko ya uunganishwaji wa mfumo ili kuweka udhibiti wa kuhakikisha mabadiliko sahihi na uidhinishwaji wa ada katika mfumo.

4.13 Bili ambazo hazikutozwa na Upotevu wa Mapato katika Mfumo wa MAJI IS

Ukaguzi wa mfumo wa MAJI IS ulibaini mapungufu katika kushughulikia wateja wanaokabiliwa na hali tofauti tofauti, hii ilipelekea baadhi ya wateja kutotozwa ankara na upotevu wa mapato kama ifuatavyo.

Wateja Hai ambao hawakutengenezewa ankara: Mfumo ulishindwa kutoza ankara kwa wateja hai 539 ambao kwenye mfumo hali inaonesha "hakuna usomaji" kwa mwezi Juni 2023. Wateja hawa, licha ya kutokuwa na usomaji wa mita ,hawakutengenezewa ankara kulingana na matumizi yao ya wastani ya miezi mitatu iliyopita kama miongozo inavyoelekeza.

Kutotozwa kwa Ankara kwa wateja ambayo hali ya mita inaonesha "Haijulikani": Mfumo ulishindwa kutoza Ankara kwa wateja ambao hali ya mita inaonesha "haijulikani". Hii ilisababisha matumizi ya maji mita za ujazo 8,397 kutotozwa ankara, na kusababisha upotevu wa mapato ya TZS 11,839,770.

Huduma za Maji Taka ambazo hazikutengenezewa Ankara: Wateja waliunganishwa upya kwenye huduma za maji taka walitumia mita za ujazo 54,748 za maji taka lakini hawakutengenezewa ankara kutokana na hitilafu katika mfumo. Hii ilipelekea upotevu wa mapato ya TZS 29,748,003.

Vilevile, kasoro kama hiyo iligunduliwa katika taasisi ya DAWASA, ambapo mfumo wa MAJI IS ulishindwa kutoza ankara kwa wateja ambao mita zilikuwa zinaonesha hali tofauti tofauti:

Mita zilizoshindwa kuendelea kufanya kazi(Stack meters): Mfumo ulishindwa kukokotoa tozo sahihi kwa wateja wanaotumia mita zilizoshindwa kuendelea kufanya kazi.

Mageti yaliyofungwa: Mfumo haukutengeneza ankara kwa baadhi ya wateja ambao hali ya usomaji inaonesha "geti limefungwa" hivyo kupelekea ankara zisizo sahihi.

Wateja ambao hali ya mita inaonesha "hakuna usomaji": wateja hai 98 wenye hali ya "hakuna usomaji" hawakutengenezewa ankara kulingana na matumizi ya wastani, na kupelekea kiasi cha shilingi milioni 2.92 kutotozwa.

Napendekeza kwamba MWAUWASA na DAWASA kushughulikia mapungufu yaliobainishwa ndani ya mfumo wa MAJI IS ili kuhakikisha mfumo unatengeneza Ankara kwa wateja kulingana na hali zao ili kuzuia upotevu zaidi wa mapato.

4.14 Mapungufu ya viwango vya matumizi ya maji vilivyopo kwenye mfumo

Mfumo wa MAJI IS, unaotumiwa na MWAUWASA una kasoro katika mantiki yake ya kushughulikia uunganishwaji mpya kwa mteja . Wakati huduma ya maji ya mteja inapounganishwa upya baada ya kusitishwa, mfumo unatumia usomaji wa mita siku ya kuunganishwa upya kama "usomaji uliopita" badala ya usomaji halisi wa awali kabla ya kusitishwa kwa huduma. Hii imepelekea ankara zisizo sahihi kwa wateja 1295.

Ninapendekeza kwamba MWAUWASA: (a)iboreshe mfumo ili kutatua changamoto (b) ihesabu upya ankara kwa wateja walioathiriwa kulingana na matumizi yao sahihi ya maji; na (c) ihuishe taarifa za wateja na taarifa za fedha ili kuakisi taarifa sahihi za ankara.

4.15 Ada za usajili hazijaingizwa katika mfumo unaohusiana na masuala ya hali ya hewa

Mfumo unaohusika na masuala ya Hali ya Hewa (Integrated Weather Portal) unaotumiwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), haujawezeshwa kukusanya ada za usajili kwa vituo vya hali ya hewa. Hii inatokana na usimamizi mdogo wa ada ndani ya mfumo. Upungufu huu unaweza kusababisha ada zisizo sahihi zinazohusiana na huduma za hali ya hewa.

Ninapendekeza kwamba TMA waingize ada zilizokosekana za usajili kwa vituo vya hali ya hewa katika mfumo.

4.16 Utozaji zaidi katika utengenezaji wa leseni mpya pamoja na vyombo vya uvuvi katika mfumo wa FiRCIS

Mfumo wa Ukusanyaji Mapato ya Uvuvi (FiRCIS), unaotumiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi hauwezi kutofautisha kati ya maombi mapya na ya kuhuisha kwa leseni hizo. Hii inapelekea, mfumo kutoza ada ya asilimia 50 kwa leseni mpya ikizichukulia kimakosa kama zimechelewa kuhuishwa.

Hii inasababishwa na mapungufu katika muundo wa mfumo usioweza kutofautisha kati ya maombi mapya na ya kuhuisha leseni. Kutoza ada ya ziada ya asilimia 50 kwa leseni mpya kunasababisha utozaji zaidi, huenda kukawakatisha tamaa waombaji leseni wapya katika sekta ya uvuvi.

Ninapendekeza kwamba Wizara ya Mifugo na Uvuvi iboreshe mfumo wa FiRCIS ili uweze kutofautisha kati ya maombi mapya na ya kuhuisha leseni.

4.17 Mapungufu katika mfumo wa SBMS yaliyopelekea kutokusanywa kwa mapato

Mfumo wa SBMS unashindwa kukokotoa kiwango cha riba katika ada zinazotokana na ucheleweshaji wa malipo ya kodi, hivyo kupelekea upotevu wa mapato ya serikali. Mfumo ulikuwa na mapungufu yafuatayo.

- **Kutotozwa kwa ada:** Mfumo ulishindwa kutoza ada kwa bili 53, yenye jumla ya Sh 361,353.22.
- **Riba Isiyosahihi:** Wateja 165 ambao hawakulipa bili kwa wakati walipaswa kutoza riba inayokua asilimia 10 kwa kila mwezi, lakini mfumo ulishindwa kutoza kiwango sahihi.

Upungufu huu unatokana na mfumo kushindwa kukokotoa kiasi cha riba. Mchakato huo unamuhitaji afisa afanye kwa mkono ambapo inaweza kupelekea makosa na kutokwa na uwiano.

Ninapendekeza TASAC iboreshe mfumo wa SBMS ili uweze kutoza riba na maduhuli kiotomatiki tarehe ya mwisho.

4.18 Utoaji leseni usioidhinishwa na mfumo kushindwa kutofautisha kati ya mizigo na vifurushi

Nimebaini mapungufu katika utoaji wa leseni na kuruhusu usafirishaji wa vifurushi vilivyozidi ukomo wa uzito uliowekwa.

Mfumo wa FiRCIS unaotumiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi - Sekta ya Uvuvi ulishindwa kuzuia utoaji wa leseni maalumu 14 zilizozidi kikomo cha kilogramu 7 kilichowekwa na Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009. Hii inaweza kupelekea ukiukwaji wa kanuni zilizowekwa kusimamia masuala ya uvuvi.

Katika Mfumo wa Usimamizi wa Mizigo wa ATCL, mfumo uliruhusu kuingizwa kwa vifurushi 2,591 vinavyozidi uzito wa kilogramu 16 uliokuwepo kwenye sera za ATCL. Hii ilisababisha malipo yasiyo sahihi ,hivyo kukiuka mwongozo wa usimamizi wa taasisi.

Matukio yote yanatokana na kasoro ya ukosefu wa ufanisi katika uhakiki wa uzito wa bidhaa katika mifumo.

Ninapendekeza:

a) Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi) iimarisha udhibiti wa mfumo katika kuhakikisha vibali maalumu havitolewi kwa mazao ya uvuvi yenye kuzidi kilogramu saba.

b) ATCL ihakikishe kuwa mfumo unauwezo wa kutofautisha kati ya mizigo na vifurushi ili mizigo itozwe tozo stahiki .

4.19 Tozo zinazopita kiasi na bili zisizo na uwiano katika kuhuisha leseni

Mfumo wa GLICA, unaotumiwa na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha ya Tanzania, ulikuwa na mapungufu kadhaa katika utengenezaji wa ada za uhuishaji wa leseni. Hasa, ukaguzi wangu ulibaini yafuatayo:

Malipo yasiyo ya Kawaida: Kwanza, leseni 2,108 zilikuwa na malipo yanayotofautiana na viwango vilivyowekwa kwenye mfumo. Pili, leseni 1,163 zilizotolewa kwa wafanyakazi wa kudumu na wasaidizi ambapo zimetozwa kinyume na kiwango kilichotakiwa.

Malipo yasiyosahihi ya adhabu: malipo 742 ya adhabu ya kuchelewa kuhuisha leseni yalipelekea malipo yaliyozidi yenye thamani ya TZS 379,320,125.

Mapungufu haya yanatokana na changamoto ya kanuni ya uhuishaji wa Leseni ndani ya mfumo wa GLICA.

Mapungufu haya yamepelekea (a) Wamiliki wa leseni kulipa zaidi kuliko ilivyokusudiwa kwa uhuishaji na adhabu; (b) Kutofuata miundo ya malipo iliyowekwa; na (c) Utozaji wa bili zisizo sahihi ambazo zinaweza kusababisha malipo pungufu.

Ninapendekeza Bodi ya Michezo ya Kubahatisha ya Tanzania ichukue hatua za haraka kuchunguza na kurekebisha mipangilio ya mfumo wa GLICA ili kurekebisha makosa yanayochangia malipo ya ziada kutokana na adhabu na kuhakikisha kuwa leseni zote zilizorudishwa zinalipiwa kulingana na viwango vilivyowekwa.

4.20 Kutokuwepo kwa mgawanyo wa majukumu katika mifumo ya mapato

Ukaguzi wangu wa mifumo ya mapato inayotumiwa na TASAC, TPA, TMDA, na LATRA ulibaini kuwepo kwa mapungufu ya mgawanyo wa majukumu juu ya mlolongo wa utengenezaji wa bili kwenye mifumo.

Tathmini ilibaini kua, mtu mmoja anafanya majukumu ya kuanzia kuunda na kuidhinisha kwa pamoja kwenye michakato mbalimbali ndani ya mfumo:

- Maombi ya vyeti 2,398 katika mfumo wa MASSEMS (mtu huyo huyo alifanya kazi kama muundaji na mthibitishaji)
- Maombi ya vyeti 6,432 katika mfumo wa SBMS
- Ankara 152 katika mfumo wa TOS unaotumika TPA (mtu huyo huyo alifanya kazi kama muundaji na mthibitishaji)
- Maombi ya leseni za PSV katika RRIMS (mtu huyo huyo alifanya kazi kama mhakiki na mthibitishaji)
- Vyeti vya majaribio ya kitabibu katika RIMS (mtu huyo huyo alifanya kazi kama mthibitishaji na mwamuzi)

Kutokuwepo kwa mgawanyo wa majukumu kunatokana na udhibiti mdogo wa kuthibitisha haki zinazotolewa kwa watumiaji.

Hali hii inaongeza uwezekano wa watu kuwa na haki nyingi kwenye mfumo, ambayo hupelekea hatari ya usalama na uadilifu wa ndani ya mfumo.

Ninapendekeza kwamba TASAC, TPA TMDA, na LATRA zichukue hatua za kuboresha mifumo ya MASSEMS, SBMS, RIMS, RRIMS, na TOS ili kuhakikisha kuwepo na mgawanyo wa majukumu pia mfumo usiruhusu mtu mmoja kufanya kazi ya kuunda na kuidhinisha maombi au nyaraka.

4.21 Mapungufu katika udhibiti wa uthibitishaji

Ukaguzi wangu wa mifumo inayotumiwa na TAMISEMI, LATRA, na TSN ulibaini mapungufu ya mifumo katika kuhakiki usahihi wa taarifa zinazoingizwa na mapungufu katika uingizaji wa taarifa zenyewe kama ifuatavyo:

- Katika mfumo wa iCHF-IMIS unaotumiwa na Ofisi ya Rais TAMISEMI, wanachama 89 na 314 katika mikoa ya Kigoma na Arusha, mtawalia, waliwezesha katika mfumo kuweza kupata kibali cha kupata huduma za afya pamoja na kwamba walikua hawajafanya malipo, Hii ilipelekea wanachama hao kuendelea kutumia huduma bila kukamilisha malipo. Aidha, kulikuwa na wanachama 739; 13209; 42803; 1783 na 1366 waliojiandikisha na CHF katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam,

Dodoma, Kigoma, na Mbeya, mtawalia, ambao walikuwa na kipindi cha uhalali kilichoziidi miezi 12.

- Katika mfumo wa RRIMS unaotumiwa na LATRA; leseni 32 za muda mfupi zilitolewa kwa wateja dhidi ya tarehe isiyo sahihi ya kikomo cha muda. Hii ilisababisha leseni zilizopita muda kuonekana kuwa halali.
- Mfumo uitwao Circulation unaotumiwa na TSN haukuwa na udhibiti wa kuhakiki idadi ya magazeti yaliyorejeshwa. Mfumo ulikua unaruhusu maafisa kuingiza idadi kubwa ya magazeti kuliko yaliyotolewa kwa wasambazaji, hivyo kuathiri bili na malipo ya wasambazaji.
- Katika mfumo wa FiRCIS unaotumiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi - Sekta ya Uvuvi, nilibaini visa vitatu ambapo mfumo uliruhusu leseni moja kutumika kuombea vibali kwa makampuni mawili tofauti, hivyo kusababisha hasara ya mapato ya dola za Kimarekani 800 kwa wizara.
- Katika mfumo wa e-VISA unaotumiwa na Idara ya Uhamiaji, nilibaini matukio 11 ambapo VISA mbili za aina moja zenye nambari tofauti lakini zikiwa na kipindi sawa cha uhalali zilitolewa kwa mtu mmoja.
- Katika Mfumo wa Usajili Mtandaoni (ORS) unaotumiwa na TIRA, nilibaini matukio 35 ambapo cheti kimoja cha leseni kilikua kinatolewa kwa watoa huduma za bima wengi. hii ilipelekea hasara ya fedha taslimu kiasi cha Sh 55,775,000.
- Katika mfumo wa “Tanzania National Business Portal” inaotumiwa na BRELA, leseni 6 za biashara zenye nambari sawa zilitolewa kwa shughuli tofauti za biashara.

Ninapendekeza kwamba Menejimenti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI, LATRA, TSN, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, BRELA, Idara ya Uhamiaji, na TIRA ziboreshe udhibiti katika mifumo ili kuhakikisha udhibiti sahihi wa uingizaji wa taarifa na uchakataji wake, hivyo kuzuia kujirudia kwa mapungufu yaliyobainika. Aidha, TAMISEMI inapaswa kufanya mapitio na kuboresha taarifa za uanachama wa bima ya afya ili kuonesha kwa usahihi hali ya uchangiaji malipo ndani ya mfumo wa ICHF-IMIS.

4.22 Mapungufu ya mfumo katika kuhakiki taarifa zinazolingizwa

Ukaguzi wangu wa mifumo inayotumiwa na Wizara ya Ujenzi, TMDA, Wizara ya Kilimo, OUT, na TSN ulibaini mapungufu juu ya udhibiti unaofanywa na mifumo kama ifuatavyo:.

- Mfumo wa Usimamizi wa Biashara ya Kilimo (ATMIS) unaotumiwa na Wizara ya Kilimo hauwezi kutofautisha sarafu (Sh/Dola ya kimarekani) iliyotumika katika kutengeneza bili. Hii ilipelekea makosa katika baadhi ya bili zilizotengenezwa kwasababu mfumo ulikua haubadili kiasi kilicho

katika bili kuendana na viwango vya mabadilishano ya fedha. Hii ilipelekea malipo pungufu ya Sh 2,005,000.

- Katika mfumo wa SARIS unaotumiwa na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, rekodi za wanafunzi 27 wa shahada ya kwanza na 6 wa shahada ya uzamili kwa mwaka wa masomo wa 2022/23 hazikuwepo kwenye orodha za waombaji. Hii inaweza pelekea kuingizwa kwa wanafunzi wasio na vigezo na uwezekano wa hasara ya kifedha kutokana na kutolipwa ada ya udahili.
- Katika mfumo uitwao Circulation unaotumiwa na TSN, kulikuwa na changamoto ya kuhakikisha uwiano wa bili kwa wateja waliopokea huduma za aina moja, hii ilipelekea mfumo kuruhusu malipo yaliyozidi na malipo yaliyopungufu yatokanayo na uuzaji wa magazeti. Tatizo hili linatokana na muundo usiojitosheleza wa mfumo unaoruhusu punguzo ambazo hazikuidhinishwa na kuingizwa kwa mkono. Hivyo mfumo uliruhusu jumla ya malipo yaliyozidi ya jumla ya Sh 45,183,960, na malipo yaliyopungufu ya Sh 1,092,865.

Ninapendekeza:

(a) Menejimenti ya Wizara ya Kilimo iboresha udhibiti wa ATMIS ili kuhakiki kiwango cha malipo.

(b) Menejimenti ya OUT iboresha udhibiti wa SARIS katika mchakato wa maombi, uteuzi, na udahili kuhakikisha kwamba wanafunzi wanaostahili pekee ndio wanaokubaliwa.

(c) Menejimenti ya TSN iboresha udhibiti wa mfumo wa Circulation kwa kuhakiki kiasi cha magazeti yaliyorudi zaidi ya kiwango kilichotengwa na kuanzisha utaratibu wa kuidhinisha kiasi kilichoripotiwa cha magazeti yaliyorudi.

4.23 Mapungufu ya ukokotoaji yaliyobainika katika mifumo

Uchunguzi wangu wa mfumo uitwao FiRCIS katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi-Sekta ya Uvuvi, na mfumo uitwao MAJI IS katika Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza na Dar es Salaam ili kutathmini usahihi katika kukokotoa ulibaini yafuatayo;

- Katika mfumo wa FiRCIS, niligundua udhibiti mdogo katika kufanya mabadiliko ya viwango vya kubadilisha fedha za kigeni na ada za malipo ya tozo za uuzaji wa samaki nje ya nchi, ambazo zilipelekea kutengenezwa kwa ada zisizo sahihi. Hii imesababishwa na mapungufu

katika muundo wa mfumo ambao haukuzingatia uthibitishaji wa taarifa zinazolingizwa. Hii ilipelekea malipo pungufu ya Sh 510,800 kwa vibali 20 vya uuzaji nje ya nchi, na malipo yaliyozidi ya Sh 55,700 kwa vibali sita.

- Katika mfumo wa MAJI IS unaotumiwa na MWAUWASA, wateja 1,994 walitengenezewa ankara za maji taka zisizosahihi, hii ilipelekea hasara ya mapato ya TZS 22,952,882. Zaidi ya hayo, DAWASA ilibadili mita 870 za wateja bila malipo, Hii ilipelekea malipo yasiyolipwa ya Sh 43,450,000. Zaidi ya hayo, mfumo haujajengwa na uwezo wa kuzuia uunganishaji wa wateja wapya ambao hawajakamilisha malipo, Hii ilipelekea malipo pungufu ya Sh 1,915,536,123.06 kati ya Septemba na Juni.

Ninapendekeza kwamba uongozi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi-Sekta ya Uvuvi, kuboresha udhibiti katika uhuishaji wa tozo za uuzaji nje. Aidha, MWAUWASA na DAWASA wanapaswa kushirikiana na Wizara ya Maji kuboresha mfumo wa MAJI IS ili kuwa na bili sahihi. Zaidi ya hayo, wanapaswa kuimarisha udhibiti ili kuhakikisha kunatolewa idhini sahihi kabla yakubadilisha mita na uhakiki wa malipo kwa uunganishaji mpya, huku wakichukua hatua za kurejesha madeni ambayo hayakulipwa kutoka kwa wateja.

4.24 Kutopatikana ripoti muhimu katika mifumo

Mapitio yangu ya mifumo ya MASSEMS, M-BILL, Integrated Weather Portal, ORS, na WIMS yalibaini kwamba mifumo hii inakosa ripoti muhimu. Ripoti zinazokosekana ni kama zinavyofafanuliwa hapa chini:

- Mfumo wa MASSEMS unaotumiwa na TASAC haujumuishi ripoti ya ukusanyaji wa mapato, ripoti ya leseni zilizotolewa, ripoti za maombi yaliyowasilishwa, na ripoti ya meli zilizosajiliwa.
- Mfumo wa M-BILL unaotumiwa na TASAC haujumuishi Ripoti ya Watoa Huduma Waliosajiliwa, ripoti ya ukusanyaji wa mapato, Ripoti ya Usafirishaji, Ripoti ya kodi ya robo mwaka, Ripoti kwa Mashirika/Makampuni yanayobadilisha Jina, au Ripoti ya Kila Mwezi ya orodha ya shehena zilizokua ndani ya meli.
- Mfumo wa Integrated Weather Portal unaotumiwa na TMA haujumuishi ripoti muhimu kama vile orodha ya vituo vya hali ya hewa vilivyosajiliwa, orodha ya vibali vilivyotolewa kwa ajili ya utoaji wa huduma za hali ya hewa, na daftari la wadau wote (wachimbaji wa madini, kandarasi, wakulima, na baharia) wanaohitaji tabiri za hali ya hewa kutoka TMA.

- Mfumo wa Usajili kwa njia ya mtandao unaotumiwa na BRELA haujumuishi ripoti inayoonesha ada za kila mwaka ambazo hazijalipwa na wateja.
- Mfumo wa CIMIS unaotumiwa na CRB haujumuishi ripoti ya muhtasari inayoelezea jumla ya ukaguzi uliofanywa ndani ya kipindi maalumu, ikiwa ni pamoja na mikoa au maeneo ya miradi.
- Mfumo wa WIMS unaotumiwa na OSHA haujumuishi ripoti inayoonesha maeneo ya kazi na miradi ambayo haikulipia ukaguzi wa hali na ufanisi wa wafanyakazi na ukaguzi wa jumla wakati wa mchakato wa usajili.

Mapungufu haya yamesababishwa na kukosekana kwa ukusanyaji wa mahitaji ya kutosha wakati wa hatua za awali za uundaji wa mifumo. Nina mashaka kwamba mapungufu haya yiliyobainika yanakwamisha uwezo wa uongozi kupata taarifa kwa wakati unaofaa kwa ajili ya kufanya maamuzi sahihi.

Ninapendekeza uongozi wa TASAC, TMA, BRELA, CRB, na OSHA kukusanya, kukagua, na kutengeneza ripoti muhimu za mifumo ambazo zitasaidia katika kufanya maamuzi.



SURA YA TANO

MFUMO WA USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU NA MISHAHARA

5.0 Utangulizi

Mfumo wa usimamizi wa Rasilimali Watu na Mishahara hufanya kazi za usimamizi wa nguvukazi, ikiwa ni pamoja na usimamizi wa taarifa za wafanyikazi, na ulipaji wa mishahara. Kutumia mfumo hii husaidia serikali kuboresha ufanisi, utiifu wa kanuni, usahihi wa taarifa na ugawaji wa rasilimali.

Katika ukaguzi wangu wa mfumo ya rasilimali watu na mishahara, kimsingi nilijikita katika kutathmini ufanisi wa udhibiti wa mfumo katika mfumo ya HCMIS, Microsoft Navision unayotumiwa na TANAPA, na SAGE PASTEL unayotumiwa na ATCL. Nilikagua vipengele muhimu kama vile udhibiti wa uthibitishaji na uchakataji, makato ya mishahara ya wafanyakazi, kupandisha cheo na kushushwa cheo kwa mfanyakazi, na utekelezaji wa mgawanyo wa majukumu katika mchakato wa ulipaji wa mishahara. Katika ukaguzi wangu, nilibaini mapungufu yafuatayo:

5.1 Udhibiti usiotosheleza wa kiwango cha chini cha mishahara

Ukaguzi wangu wa HCMIS, na Microsoft Navision, ulibaini kutokuwepo na udhibiti wa kutosheleza wa kuzuia wafanyakazi kupata chini ya theluthi moja ya mishahara wao baada ya makato. Hii ilisababisha wafanyakazi kupata chini ya kiwango kwenye kila mfumo. Makato yasiyo sahihi yanaweza kusababisha kutofuata sheria na kanuni za kazi, na hivyo kusababisha madhara ya kisheria na kifedha.

Ninapendekeza kwamba uongozi wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (PO-PSMGG) na TANAPA waimarishe udhibiti wa mfumo ili kuhakikisha makato yanazingatia kanuni zilizowekwa.

5.2 Mapungu ya makato ya mishahara katika mfumo wa Sage Pastel

Ukaguzi wangu wa mfumo wa Sage Pastel unaotumiwa na ATCL ulibaini mapungufu katika makato ya mishahara. Ambapo Watumishi 10 walikuwa na makato ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (SSF) yanayozidi 5%, Watumishi watatu walikuwa na tofauti katika makato yao ya HESLB, huku mishahara ikitwa chini ya 15% iliyokusudiwa kwa baadhi, huku wengine wakikatwa zaidi ya hapo.

Hii ilisababishwa na udhibiti mdogo wa muundo wa mfumo ambao haukuweza kuhakikisha makato yanafanywa kwa usahihi kulingana na kanuni.

Matokeo yake, makato makubwa ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii yanaweza kuwasababishia wafanyakazi matatizo ya kifedha. Changamoto za makato ya HESLB yanaweza kuvuruga ulipaji wa mkopo, na kuathiri fedha za wafanyakazi.

Ninapendekeza Uongozi wa ATCL: (a) Kuimarisha udhibiti wa mfumo wa makato ya mishahara, kutekeleza ukaguzi wa uthibitishaji na kuhakikisha matumizi sahihi ya viwango vya makato kwa PSSSF na HESLB ; na (b) Kufanya mapitio ya mara kwa mara na upatanisho wa orodha ya mishahara ili kufanikisha uzingatiwaji wa sheria na usahihi katika mchakato wa makato.

5.3 Mapungufu juu ya mgawanyo wa majukumu katika mfumo wa HCMIS

Ukaguzi wa mfumo wa HCMIS ulibaini ukosefu wa utendakazi wa idhini ya kubadilisha tarehe ya kuzaliwa ya mfanyakazi na kurekebisha bajeti za mishahara(PE). Mtumiaji mmoja tu kutoka PO-PSMGG anaweza kubadilisha maelezo haya.

Hii ilisababishwa na muundo wa mfumo usiotosha ambao umeshindwa kujumuisha mtiririko unaofaa katika kuidhinisha. Mtumiaji mmoja anayefanya kazi muhimu za Utumishi huongeza hatari ya makosa ambayo hayajatambuliwa na shughuli zisizoidhinishwa.

Ninapendekeza kwamba menejimenti ya PO-PSMGG kuimarisha mfumo kwa kujumuisha mtiririko wa uidhinishaji uliopangwa kwa ajili ya kudhibiti mabadiliko ya tarehe ya kuzaliwa ya mfanyakazi na uthibitishaji wa bajeti ya mishahara.

5.4 Masuala ya usimamizi katika upandishaji na ushushaji wa madaraja katika HCMIS

Mapitio yangu ya mfumo wa HCMIS, nilibaini mapungufu katika kusimamia upandishaji wa madaraja kwa wafanyakazi. Hii ilisababisha:

- Wafanyakazi 487 walipata mabadiliko yasiyotarajiwa ya upandaji daraja wakati wa mchakato wa kawaida wa upandishaji vyeo
- Watumishi 248 hawana kumbukumbu zinazobainisha daraja walilopandishwa.
- Wafanyakazi 20 walipandishwa vyeo bila kukidhi mahitaji ya chini ya miaka mitatu.
- Watumishi 10 walioshushwa vyeo ambao mishahara yao haikubadilishwa.

Hii ilisababishwa na mfumo kutokuwa na udhibiti wa kutekeleza mahitaji ya chini ya umiliki na kuhakikisha marekebisho ya mishahara baada ya kushushwa vyeo.

Usimamizi mdogo wa upandishaji na ushushaji wa madaraja husababisha upotevu wa fedha kutokana na malipo yasiyo sahihi ya mishahara.

Ninapendekeza kwamba Usimamizi wa PO-PSMGG Uimarise mfumo wa HCMIS kwa kutekeleza (a) utendakazi kiotomatiki unaosababisha marekebisho ya mishahara baada ya kuidhinishwa kwa ushushaji vyeo (b) Udhibiti wa kuzuia na kuthibitisha upandishaji vyeo wa kawaida, kuzuia watu wasiostahiki kupandishwa vyeo na kuruka hatua za daraja la mishahara.

5.5 Hesabu isiyo sahihi juu ya malipo ya posho ya masaa ya ziada

Ukaguzi wa mfumo unaotumika kushughulikia maombi ya posho (MIS) nilibaini kuwepo kwa hitilafu katika jinsi ya kukokotoa posho za maombi 26. Hitilafu hizi zilisababisha kiasi kilichokokotolewa cha mfumo kuwa tofauti na matokeo niliyopata kupitia ukaguzi.

Hii ilisababishwa na mantiki (logic) ya ukokotoaji katika mfumo kukosa ufanisi katika kuleta matokeo yaliyo sahihi, Makosa katika ukokotoaji yamesababisha masuala ya kifedha kwa wafanyakazi na shirika.

Ninapendekeza kwamba Bodi ya Mfuko wa Barabara ibadilishe vidhibiti vya kukokotoa katika eneo hili la posho ili kuhakikisha ukokotoaji sahihi.

5.6 Mkopo wa wafanyakazi unaovuka kikomo cha TZS 1,000,000

Mapitio yangu ya mikopo ya watumishi iliyotolewa kwa watumishi wa TANAPA yalibaini watumishi 19 waliopata mikopo inayovuka TZS 1,000,000 ukomo uliowekwa na kanuni.

Kuzidisha kikomo cha mkopo kunaweza kutatiza upangaji na ugawaji wa bajeti, na hivyo kuwanyima wafanyakazi wengine wanaostahiki mikopo.

Ninapendekeza TANAPA iimarise udhibiti wa mfumo ili kuzuia utoaji wa mikopo kwa watumishi zaidi ya ukomo uliotajwa.

5.7 Mapungufu ya mfumo katika usimamizi wa likizo za watumishi

Ukaguzi wangu ulibaini mapungufu katika mfumo juu ya usimamizi wa likizo katika mashirika mbalimbali:

- **HCMIS:**Wafanyakazi 34 waliokuwa kwenye likizo bila malipo walijumuishwa kimakosa kwenye orodha ya malipo na kupokea mishahara.

- **ERMS (eGA):**Mfumo huo unaruhusu mkusanyiko wa likizo unaozidi miaka miwili, kinyume na kanuni. Nilipata wafanyakazi 153 wakiwa na likizo iliyoongezwa iliyoziidi kikomo.
- **PMIS (TPC):**Niliona ufuatiliaji usio sahihi na hesabu ya muda wa likizo.

Hii ilisababishwa na muundo mbovu wa mfumo ambao ulishindwa kuhakikisha usimamizi wa likizo unalingana na kanuni.

Mapungufu haya yalisababisha: (a) Utoaji wa mishahara usio sahihi kwa wafanyakazi kwenye likizo bila malipo; (b) Mkusanyiko wa likizo inayozidi kikomo cha miaka miwili; na (c) Ufuatiliaji na ukokotoaji usio sahihi wa muda wa likizo.

Ninapendekeza kwamba PO-PSMGG, e-GA, na TPC kuboresha utendajikazi juu ya likizo katika mfumo wa usimamizi wa watumishi. Hii ni pamoja na: (a) Kuondoa kiotomatiki wafanyakazi walio na likizo iliyoidhinishwa bila malipo kutoka kwa orodha ya malipo ya mishahara; na (b) Kufuatilia na kukokotoa kwa usahihi siku za likizo za mfanyakazi kwa mujibu wa kanuni za kudumu za utumishi wa umma.

5.8 Nambari za watumishi (check number) na nambari ya kidato cha nne zinazofanana katika mfumo wa HCMIS

Ukaguzi wangu wa HCMIS ulibaini kuwepo kwa tatizo katika uthibitishaji wa taarifa za wafanyakazi:

- a) Baadhi ya wafanyakazi wamepewa nambari nyingi za utumishi wa umma, jambo ambalo linaweza kusababisha mgongano au makosa katika uchakataji wa malipo.
- b) Wafanyakazi 238 wanashiriki nambari sawa za kidato cha nne.

Hii ilisababishwa na uthibitisho usio sahihi na usiofaa wa taarifa za mfanyakazi wakati wa mchakato wa kuajiri. Taarifa ya nakala huhatarisha uaminifu wa taarifa na huzuia utambuzi sahihi wa wafanyakazi binafsi.

Ninapendekeza kwamba PO-PSMGG iongeze mantiki na mbinu za uthibitishaji katika mfumo ili: (a) Kuzuia ugawaji wa nambari nyingi za utumishi wa umma kwa mfanyakazi mmoja; (b) Kuunganishwa na mfumo wa NECTA wa uhakiki na uthibitishaji wa nambari za kidato cha nne kwa watumishi wapya.

SURA YA SITA

USIMAMIZI WA MIFUMO

6.0 Utangulizi

Usimamizi wa mifumo, unahusisha usimamizi wa akaunti za watumiaji, udhibiti katika kutoa haki za utumiaji wa mifumo, utekelezaji wa usalama wa mifumo, na kutatua changamoto za mifumo, na unahakikisha uendeshaji wenye ufanisi na salama wa mifumo katika taasisi.

Ukaguzi wa udhibiti wa usimamizi wa mifumo uliofanywa katika taasisi mbalimbali za serikali ulibaini matokeo yafuatayo: Haki za utumiaji wa mfumo zilizopitiliza zilitolewa kwa maafisa wa TEHAMA, Kuvunjika kwa itifaki katika utekelezaji wa majukumu, na Uwepo wa haki za kutumia mifumo na kanzidata usiodhibitiwa kwa wazabuni wa mifumo.

6.1 Haki za utumiaji wa mifumo uliopitiliza kwa Maafisa wa TEHAMA

Ukaguzi wangu katika taasisi mbalimbali za serikali umebaini mapungufu kuhusu utoaji wa haki za utumiaji wa mifumo kwa maafisa wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Mapungufu haya yanabainisha hatari katika usalama wa mifumo, ambao unaweza kuhatarisha usalama wa taarifa na ufanisi wa utendaji kazi.

Ifuatayo ni mifano maalum iliyobainishwa wakati wa ukaguzi:

- Uchambuzi wa Mfumo wa “RIMS” unaotumika katika Mamlaka ya Udhibiti wa Madawa na Vifaa Tiba (TMDA), ulibainisha kwamba maafisa wa TEHAMA wana haki zilizopitiliza za utumiaji wa mifumo, ambapo iliwaruhusu kuepuka hatua muhimu wakati wa kutoa vyeti vya usajili wa bidhaa. Hatua hizo ni kama vile kutengeneza ankara na kuidhinisha, hivyo kurahisisha kuwasilisha maombi moja kwa moja kwenye hatua ya mwisho bila kupitia hatua hizo tajwa.
- Katika Mfumo wa “BCMS” ambao unatumika na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), maafisa wa TEHAMA walipewa haki zilizopitiliza za utumiaji

wa mifumo. Hii imepelekea kuweza kutengeneza na kufuta ankara, pamoja na kusajili magari, ambayo ni kinyume na majukumu yao yaliyowekwa.

- Maafisa tisa wa TEHAMA wa Ofisi ya Rais TAMISEMI walipewa majukumu ya watu wa idara ya fedha katika mfumo wa TAUSI ambayo ingewawezesha kutumia vibaya mamlaka hiyo.
- Maafisa wa TEHAMA wa eGA walioainishwa kwa lengo la kuhamisha maarifa na kutoa msaada wa kiufundi kwa mfumo wa ERMS walipewa majukumu ya maafisa wa biashara, yanayojumuisha maeneo kama uhasibu, manunuzi, na usimamizi wa magari.
- Mchambuzi wa mifumo ya kompyuta aliingiza taarifa za wafanyakazi kwenye Mfumo wa Taarifa za Usimamizi (MIS) unaotumiwa na Bodi ya Mfuko wa Barabara badala ya afisa wa rasilimali watu.

Mapungufu haya yamesababishwa na uhibititi mdogo wa utoaji wa haki za utumiaji wa mifumo na kukosekana kwa mgawanyo wa majukumu. Hii inapelekea ufanisi mdogo wa uwajibikaji, tofauti za taarifa, hatari za usalama na athari za kifedha.

Ninapendekeza uongozi wa serikali Mtandaoni, Ofisi ya Rais TAMISEMI, NSSF, TMDA, na Bodi ya Barabara kufanya tathmini upya na kurekebisha haki za kutumia mifumo kwa maafisa wa TEHAMA ili ziendane na majukumu yao.

6.2 Marekebisho ya faini na adhabu kwenye kanzidata na maafisa TEHAMA wanaohusika kusimamia kanzidata

Faini zinazokusanywa kupitia Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Reli na Barabara (RRIMS) haziwezi kulipwa mara baada ya nambari ya uhibititi kumalizika muda wake. Chaguo pekee ni kulipa kupitia nambari mpya ya uhibititi iliyozalishwa katika mfumo tofauti unaoitwa “GePG Generic portal”. Hata hivyo, RRIMS haijaunganishwa na “GePG Generic portal” ili kusasisha moja kwa moja hali ya faini kama imelipwa. Ili kukamilisha malipo, afisa TEHAMA msimamizi wa kanzidata anahitaji kusasisha hali ya nambari ya awali (iliyomalizika muda wake) katika kanzidata ya RRIMS kuwa imelipwa.

Mchakato huu unaweka hatari ya marekebisho yasiyoruhusiwa kwa miamala ambayo haijafanyiwa malipo na afisa TEHAMA wasimamizi wa kanzidata, bila kuwepo kwa uhibititi kama vile taratibu za idhini au ukaguzi wa mara kwa mara wa shughuli zinazofanywa kwenye mfumo.

Ninapendekeza kwamba uongozi wa LATRA:

- (a) Kuboresha mfumo wa RRIMS ili kiotomatiki kutengeneza namba za udhibiti kwa makosa yaliyochelewa malipo. Hii itapunguza mlolongo wa malipo na kutokomeza haja ya msimamizi wa kanzidata kufanya marekebisho kwa kupitia kanzidata.
- (b) Kukagua na kufuatilia mara kwa mara shughuli zinazofanywa na akaunti za msimamizi wa kanzidata ili kuhakikisha usahihi wa marekebisho.

6.3 Haki za utumiaji wa mifumo usiodhibitiwa kwa wazabuni wa mifumo katika mfumo wa usimamizi wa ruzuku

Ukaguzi wa Mfumo wa Usimamizi wa Ruzuku wa TFRA ulibaini kuwa mzabuni anashikilia haki za utumiaji wa mfumo usiodhibitiwa kwenye seva na kanzidata, ambayo ni kinyume na taratibu. Hii inaleta hatari za usalama wa taarifa. Aidha, maafisa wa TEHAMA wa TFRA hawawezi hata kutoa taarifa kutokana na haki hafifu walizonao, hii ikionesha utumiaji wa mifumo usioruhusiwa au uvunjaji wa usalama.

Haki za utumiaji wa mifumo usiodhibitiwa katika seva na kanzidata husababisha hatari kama vile taarifa inaweza kunakiliwa, kusambazwa, au kutumiwa vibaya na mzabuni au wafanyakazi wake.

Ninapendekeza kwamba TFRA: (a) Ipokonye wazabuni haki za utumiaji wa mifumo katika seva na kanzidata; na (b) Ibainishe na kurekodi akaunti zote zenye haki ya kufikia na kutumia seva na kanzidata.

6.4 Ufanisi mdogo juu ya udhibiti wa upatikanaji wa haki za kutumia mfumo katika Mfumo wa usimamizi wa mizigo

Ukaguzi wa mifumo ya usimamizi wa mizigo ya ATCL ulibaini kwamba ATCL haina haki za kutumia mfumo katika kipengele cha kubadilisha viwango vya ubadilishaji wa sarafu na utengenezaji wa akaunti za watumiaji; hii husababisha kutegemea mawasiliano ya barua pepe na wazabuni wa mfumo huo ambao huzisasisha viwango hivi kwa niaba.

Hii imesababishwa na usimamizi usiotosheleza wa utoaji wa haki za kutumia mifumo, ambao haukuzingatia mgawanyo wa majukumu haya kwa uongozi wa ATCL.

mapungufu haya husababisha usumbufu wa uendesaji, ukipelekea kwa kucheleweshwa katika kusasisha kiwango cha kubadilisha fedha na utengenezaji wa akaunti za watumiaji.

Ninapendekeza bodi ya ATCL ipitie makubaliano ya kiwango cha huduma (SLA) na mzabuni, na kuhakikisha kuwa majukumu, ikiwa ni pamoja na kusasisha viwango vya ubadilishaji wa fedha za kigeni na uundaji wa akaunti za watumiaji, zinahamishiwa ATCL.



SURA YA SABA

UBORESHAJI WA MIFUMO NA UENDESHAJI WA KIOTOMATIKI

7.0 Utangulizi

Ili kufikia ubora wa uendeshaji katika sekta ya umma kunahitajika tathmini ya utekelezaji wa mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na uendeshaji wa kimkakati wa kiotomatiki. Sura hii inabainisha hali ya sasa ya kiotomatiki katika taasisi mbalimbali za serikali, ikizingatia kiwango cha ujumuishaji (*systems integration*) wa mifumo, matumizi bora ya teknolojia, na uwezo wa mageuzi ambao huletwa na Mifumo ya TEHAMA iliyoboreshwa kwa taasisi zilizo chini ya ukaguzi wa sekta ya umma.

7.1 Ukosefu wa ujumuishaji kati ya mifumo ya bili na GePG

Ukaguzi wa mtiririko wa shughuli za taasisi umebaini matatizo kwenye ujumuishaji wa mifumo na GePG katika taasisi kadhaa:

- **UCSAF:** Mfumo wa SAGE evolution hauna ujumuishaji na GePG, ambayo inaweza kusababisha makosa kwenye kiasi cha bili.
- **TMA:** Mfumo wa TMA (*Integrated Weather Portal*) haujajumuishwa na mfumo wa GePG hivyo kupelekea ada kutengenezwa na afisa katika mfumo ambao umetengenezwa kutumiwa na taasisi zisizo na mfumo wa kutengeneza bili (generic GePG portal), hii hupelekea hatari ya kutengeneza ada zenye makosa kwasababu kiwango cha ada kinawekwa na afisa husika.
- **TSN:** licha ya uwepo wa mifumo kama Circula na ePaper, bili zinatengenezwa kwenye mfumo “generic GePG portal” na afisa kutokana kutojumuishwa kwa GePG engine. Pia mfumo wa e-Papper umejumuishwa na Selcom kwa ajili ya malipo kinyume na malengo ya GePG. Hii usababisha kutokuwepo kwa uwazi wa makusanyo ya serikali.

- **OUT:** Kukosekana kwa ujumuishwaji wa mfumo wa SARIS and GEPG kunapelekea uwepo wa makosa katika kutengeneza bili za ada na michango mbalimbali ya wanafunzi na kukosa ulinganifu wa taarifa baina ya mifumo hii miwili. Kwa mfano, rekodi 20 za malipo ya mitihani na malipo 40 ya ada zilikuwa kwenye mfumo na SARIS and hazipo kwenye mfumo wa malipo wa GEPG.

7.2 Tofauti ya taarifa kwenye mifumo ya bili iliyojumuishwa na GePG

Katika ukaguzi wa ujumuishaji wa GePG na mifumo mbalimbali ya bili niligundua tofauti zifuatazo katika malipo yaliyofanyika.

- **Posta Kiganjani:** Mfumo ulionesha utofauti wa taarifa za waliolipa na nambari za malipo zikiwa zimejirudia, na hivyo kusababisha uwezekano wa kupoteza mapato na changamoto katika kutoa taarifa za fedha.
- **RIMS:** Miamala yenye jumla ya Sh 1,729,407 ilikuwa na fedha kidogo zilizosajiliwa kwenye GePG ikilinganishwa na RIMS, pia muamala wenye Sh 920,000 ilikuwa na fedha nyingi zaidi kwenye GePG.
- **RITA:** Rekodi za bili 526,115 zilikuwa kwenye GePG lakini hazikupatikana katika mfumo wa bili wa RITA, pia rekodi 114 za bili zilikuwa kwenye mfumo wa RITA lakini hazikuonekana kwenye GePG.
- **Law School:** Ulinganisho wa taarifa za GePG na daftari la fedha la MUSE ulionesha miamala iliyo na tofauti za fedha, ikiwa na tofauti ya jumla ya Sh 115,644,139 kati ya mifumo miwili (Sh 3,092,299,998 zilizosajiliwa kwenye GePG na Sh 3,207,944,137 kwenye MUSE).

7.3 Ukosefu wa ujumuishaji wa mifumo

Ukosefu wa ujumuishaji kati ya mifumo mbalimbali ya TEHAMA unaathiri ufanisi, usahihi wa data, na uwazi wa taarifa za fedha, na hivyo unaweza kusababisha makosa, kutofautiana kwa taarifa, na hata hasara za kifedha.

Katika ugakuzi nilibaini maeneo mahususi ambayo ukosefu wa ujumuishaji wa mifumo unapelekea changamoto kama ifuatavyo:

- Mifumo ya usimamizi wa shughuli za taasisi na uhasibu: Sehemu hii inabainisha ukosefu wa ufanisi unaosababishwa na kutojumuishwa kwa

mifumo inayotumika kufanya shughuli kuu za taasisi na mfumo wa uhasibu unaohusika na kuandaa taarifa malipo.

- Mifumo ya bili na uhasibu: Sehemu hii inaonesha namana taarifa zinavyohamishwa na afisa kutoka kwenye mifumo ya bili kwenda kwenye mfumo wa uhasibu inavyoweza kusababisha makosa ya kibinadamu na repoti za kifedha zisizosahihi.
- Mifumo ya bili na ya uendeshaji wa shughuli za taasisi: Sehemu hii inachambua changamoto zitokanazo na ukosefu wa ujumuishaji kati ya mifumo ya bili na mifumo inayotumika kuendesha shughuli za taasisi, na hivyo kuathiri kazi kama vile uhakiki na uthibitisho wa taarifa za huduma na miamala.
- Mifumo ya uhasibu na benki: Sehemu hii inabainisha changamoto ya kutojumuishwa mifumo ya fedha na benki ambayo upelekea utofauti kati ya malipo yaliyoidhinishwa na miamala halisi ya benki kwa sababu ya kuhamisha taarifa kwa njia ya mkono (manual) katika mifumo ya kifedha na ya benki (internet banking portal)
- Mifumo ya uendeshaji wa shughuli za taasisi mbalimbali: Sehemu hii inabainisha jinsi ukosefu wa ujumuishaji kati ya mifumo ya uendeshaji wa shughuli baina ya taasisi, inavyozuia ubadilishanaji na uhakiki wa taarifa.

7.3.1 Mifumo ya usimamizi na mifumo ya uhasibu

Ukaguzi wa ujumuishaji wa mifumo inayotumika TASAF na RFB ulibaini matatizo katika utendaji kazi. Taasisi hizi utegemea mifumo tofauti (**PSSN-MIS** kwa **TASAF** na **MIS for RFB**) katika kusimamia shughuli zake kuu hasa katika hatua za mwanzo za utaratibu wa malipo. Hata hivyo, mifumo hii haina ujumuishaji na MUSE ambao ni mfumo wa msingi wa uhasibu. Ukosefu huu wa ujumuishaji unazuia uhamisho wa moja kwa moja wa taarifa za malipo, ambayo ni muhimu kwa kukamilisha malipo. Matokeo yake, lazima afisa ahamishe taarifa hizo, na hivyo kuongeza hatari ya kutofautiana katika malipo na kutokuwa na usawa katika rekodi.

7.3.2 Mifumo ya bili na mifumo ya uhasibu

Tathmini yangu kuhusu ufungamano wa mifumo iliyopo katika taasisi za TSN, ATCL, na TPDC ilibainisha ukosefu wa kufungamana kati ya mifumo yao ya bili (Circulation System, Cargo Management System, Crane Revenue System, na

LAPIS) na mfumo wao wa uhasibu wa SAGE. Matokeo yake, taasisi hizi humtegemea afisa (mfanyakazi wa taasisi husika) kuhamisha data kutoka kwenye mfumo wa bili kwenda kwenye mfumo wa uhasibu, na hivyo kuongeza hatari ya makosa ya kibinadamu wakati wa kuhamisha taarifa, hivyo inaweza kupelekea utoaji wa taarifa za fedha zisizo sahihi.

Vivyo hivyo, katika huduma za T-PESA, ukosefu wa ufungamano kati ya mfumo wa huduma za fedha kwa njia ya mkononi wa TTCL na mfumo wa ERMS unahitaji afisa husika kuingiza taarifa kwenye mfumo wa ERMS kwa ajili ya kutambua mapato. Utaratibu huu unaongeza hatari ya makosa ya kibinadamu na kutoa taarifa zisizokuwa sahihi.

7.3.3 Mifumo ya bili na mifumo ya usimamizi wa shughuli za taasisi

Ukaguzi wangu ulibainisha kuwa mfumo wa taarifa za ukusanyaji mapato ya uvuvi (FiRCIS) wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi haukufungamana na mifumo muhimu kadhaa:

- Mamlaka ya vitambulisho vya taifa (NIDA): Kutofungamana baina ya mfumo wa FiRCIS na mfumo wa vitambulisho vya taifa unazuia uthibitishaji na uhakiki wa uraia wa waombaji wa leseni za biashara ya uvuvi.
- TAUSI na BRELA: Mifumo hii ni muhimu kwa kutoa nambari za leseni za ukusanyaji wa mazao ya uvuvi, ambazo ni sharti la kupata leseni za biashara ya uvuvi. Ukosefu wa ufungamanisho huu unazuia FiRCIS kuthibitisha leseni za biashara kwa ufanisi.
- Benki Kuu ya Tanzania (BoT): Ukosefu wa kufungamana na BoT unazuia usasishaji wa moja kwa moja katika viwango vya ubadilishaji wa fedha vinavyotumika katika mahesabu ya ada za vibali na leseni za biashara ya uvuvi. Hii inaweza kusababisha kutotoza kiasi sahihi, kama ilivyothibitishwa na ukaguzi wetu ambao uligundua upungufu wa TZS 379,932 kutotozwa.

Zaidi ya hayo, mfumo wa RIMS wa TMDA unakabiliana na changamoto kama hiyo ya kutokuwa na ufungamano na mfumo wa Benki Kuu. Kutokuwepo kwa uhusiano wa moja kwa moja na Benki Kuu ya Tanzania kunazuia upatikanaji wa viwango vya ubadilishaji wa fedha kwa wakati halisi, hivyo kusababisha mipangilio isiyo sahihi ya ada na kuingilia usahihi wa malipo kamili.

7.3.4 Mifumo ya usimamizi wa uendeshaji shughuli za taasisi

Ukaguzi wangu ulibaini ukosefu wa ufungamano kati ya mifumo ya usimamizi wa shughuli za uendeshaji baina ya taasisi mbalimbali za umma hapo chini. Ukosefu huu unazuia uthibitishaji na uhakiki wa taarifa kwa ufanisi, ubadilishaji sahihi wa taarifa kati ya mifumo na taasisi mbalimbali, kama inavyoelezwa kwa kina kwenye jedwali hapa chini.

Taasisi	Mifumo Yenye Kukosa Ufungamano	Sababu ya Ufungamano	Madhara
Wizara ya Ujenzi	SPLS na Mfumo wa Maombi ya TIN wa TRA	Uthibitishaji wa moja kwa moja wa nambari za TIN kwa vibali vya mzigo maalum	Makosa na utoaji wa vibali vyenye nambari za TIN batili
OSHA	OSHA WIMS na Mfumo wa CRB	Kushirikishana kwa urahisi taarifa muhimu za mradi	Bili zisizo sahihi pamoja na upungufu/makosa katika utendaji
TASAC	SBMS pamoja na TRA, M-BILL na TRA, BRELA	Kubadilishana moja kwa moja tathmini za awali na za mwisho za bidhaa na mali zilizoagizwa, na uthibitishaji wa leseni za biashara	Makosa yanayosababisha kutokuwa sahihi kwa uthibitishaji wa leseni za biashara
	Mfumo wa Taasisi ya Bahari ya Dar es Salaam na NIDA	Uthibitisho wa cheti kiotomatiki, utoaji wa nambari za DMI, na kutambuliwa kwa uraia wakati wa usajili wa mabaharia	Makosa na kuhatarisha uadilifu wa taarifa kati ya mifumo.
Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora	HCMIS na PSRS	Kushirikishana taarifa muhimu kwa ajili ya kuweka wafanyakazi wapya na utoaji wa vibali vya kuajiri	Makosa ya kiutendaji na udanganyifu.
Idara ya Uhamiaji Tanzania	Mfumo wa Nyaraka ya Usafiri wa Dharura (ETD) na Mfumo wa Kudhibiti Usimamizi wa Mpaka (BMC) na Mfumo wa Pasipoti	Uthibitisho wa uhalali wa nyaraka na kushirikishana taarifa kiotomatiki kwa watu waliojiandikisha katika mfumo wa pasipoti, VISA na ETD	Kizuizi cha uthibitisho wa kiotomatiki wa uhalali wa nyaraka, makosa yakiutendaji, na matumizi mabaya ya taarifa.



Taasisi	Mifumo Kukosa Ufungamano	Yenye	Sababu ya Ufungamano	Madhara
Wizara ya Fedha	Dfund na NPMIS, mifumo ya benki za kibiashara, MUSE, na CBMS		Uthibitisho wa taarifa za miradi katika NPMIS, kutunza kumbukumbu za malipo ya wauzaji, uhamishaji wa moja kwa moja wa taarifa za fedha za wafadhili, na uthibitisho wa bajeti ya miradi	Makosa ya utendaji, kucheleweshwa katika kutunza kumbukumbu za malipo, na changamoto katika uthibitisho wa bajeti ya miradi
	GERAS na e-Ofisi		Uthibitisho wa kibali kutoka PST	Hatari ya kutoa fedha kwa kutokuwa na idhini au kutokuwa na usahihi wa fedha zilizoidhinishwa.
CRB	CIMIS na CMVRS na BRELA		Uthibitisho wa ufanisi wa usajili wa magari, maelezo ya mmiliki, na taarifa za kampuni wakati wa mchakato wa usajili wa mkandarasi	Upungufu wa taarifa, kuchelewa kwa usajiri, na uwezekano wa kutokuwa sahihi, unaoleta hatari kwa uaminifu wa data za mkandarasi
Chuo kikuu Mzumbe, NIT, SUA, UDOM	Mifumo ya Usimamizi wa Wanafunzi na HESLB LMS		Ufungamano kati ya mfumo wa usimamizi wa wanafunzi na mfumo wa usimamizi wa mikopo	Tofauti katika data na kuchelewa katika utoaji wa mikopo kwa wanafunzi.
NSSF	CFMS Plus na Oracle ERP		Usawazishaji wa data za wanufaikaji	Ucheleweshaji wa kusawazisha taarifa za wanufaikaji, tofauti katika taarifa za kifedha, Tathmini isiyo sahihi ya uimara wa Mfuko.
OUT	SARIS na HESLB		Kushirikishana data ya malipo ya ada za wanafunzi	Uchakataji wa taarifa kwa kumtegemea afisa uliosababisha kuchelewa kwa huduma na kuongezeka kwa uwezekano wa makosa katika

Taasisi	Mifumo Kukosa Ufungamano	Yenye Sababu ya Madhara Ufungamano	
			kuingiza data za wanafunzi.
Ofisi ya Rais TAMISEMI	CHF na FFARS/MUSE	Sasisho ya malipo ya madai yaliyotumwa kwenye mfumo wa uhasibu.	Kuingiza taarifa kwenye mfumo wa uhasibu kwa kutegemea afisa husika kunaweza kusababisha makosa na udanganyifu.
	CHF na GOTHOMIS	Uthibitisho wa hadhi ya uanachama kabla ya matumizi ya huduma ya bima	Uhakiki wa taarifa kwa kutegemea afisa husika unaweza kusababisha huduma kutolewa kwa watu wasio stahili na upotevu wa mapato ya serikali.

Ili kuboresha uwazi na ufanisi wa kutengeneza bili, na kupunguza uwezekano wa kupoteza mapato kutokana na makosa ya kibinadamu, napendekeza kuunganishwa kwa mifumo ya taasisi zilizoorodheshwa. Aidha, OSHA, TPC, NSSF, na TMDA zinapaswa kutekeleza uhakiki wa uadilifu wa data, kama vile taarifa za hapo kwa hapo ili kuondoa kutofautiana, na kuhakikisha uhamisho wa data kamili, sahihi, na thabiti.

7.4 Mifumo ya TEHAMA kutotumika kikamilifu

Tathmini yangu kuhusu utumiaji wa mifumo ya TEHAMA katika taasisi za REA, STAMIGOLD, TFRA, HESLB, TMDA, RFB, NSSF, PO-PSMGG, na Wizara ya Maji ilibainisha kuwa taasisi hizi zinatumia mifumo ya TEHAMA iliyotengenezwa ili kukidhi mahitaji ya watumiaji. Hata hivyo, niligundua kuwa uwepo wa utumiaji duni wa baadhi ya vipengele muhimu katika mifumo hii unaozuia kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa na kuathiri vibaya thamani ya fedha iliyotumika kuendeleza mifumo hii (ROI). Vipengele/moduli ambayo havifanyi kazi kikamilifu vimeorodheshwa kwenye jedwali hapa chini

Jedwali 1: Vipengele visivyotumika kikamilifu

Taasisi	Jina la Mfumo	Vipengele Kikamilifu	Visivyotumika
TMDA	RIMS	Ufuatiliaji wa bidhaa zinazoingizwa kwa masharti	



PO-PSMGG	HCMS	Ubadilishaji wa vituo vya kazi, kupanga vituo vya kazi, uhamisho, na likizo za wafanyakazi
NSSF	PMS	Usimamizi wa Matumizi ya fedha na Portal ya Wapangaji wa Mara Moja
RFB	MIS	Ufuatiliaji wa likizo za wafanyakazi
HESLB	ERP	Moduli ya utekelezaji wa sheria na taratibu za taasisi
TFRA	FIS	Ukaguzi na usimamizi wa mali
STAMIGOLD	Sage Evolution accounting system	Mradi, Mkataba, Ununuzi, Orodha ya Bidhaa, na Mali Zisizohamishika
REA	Serenic Navigator	Ufuatiliaji wa utendaji wa bajeti, rasilimali watu, manunuzi, upatanisho, oda za ununuzi, na michakato ya maombi
e-GA	ERMS	Moduli ya Kupokea Bidhaa
MOFP	Dfund	Moduli ya kuripoti matumizi ya fedha za wafadhili

Ninapendekeza taasisi hizi zichukue hatua kuhakikisha matumizi kamili ya mifumo iliyoundwa au kununuliwa. Lengo kuu la hatua hii ni kufikia matokeo yaliyokusudiwa ya kibiashara na kuhakikisha upatikanaji wa faida kutokana na uwekezaji uliofanywa.

7.5 Huduma za taasisi zisizo kwenye mifumo ya kielektroniki

Sehemu hii inawasilisha muhtasari wa kina wa matokeo ya ukaguzi uliofanywa kwa taasisi mbalimbali za serikali, na kutoa mwanga kuhusu vipengele muhimu vya michakato yao ya uendeshaji. Lengo la uchunguzi huu lilikuwa kutathmini kiwango cha utumiaji wa mifumo ya kielektroniki ndani ya taasisi hizi, ikilenga kutambua michakato isiyo ya kielektroniki na athari zake zinazowezezana kuanzia kuchunguza maelezo ya utendajikazi wa taasisi, kubainisha maeneo ambayo huduma za kielektroniki inaweza kuongeza ufanisi, usahihi na uwazi.

Ukaguzi wangu wa viwango vya kielektroniki katika taasisi za ATCL, UCSAF, TFRA, TIRA, REA, LATRA, Idara ya Uhamiaji, TPC, TASAC, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, NSSF, na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha ulibainisha michakato mbalimbali ambayo haijawekwa katika mfumo wa kielektroniki kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali hapa chini.

Jedwali 2: Huduma za taasisi zisizo kwenye mifumo ya kieletroniki

Taasisi	Huduma Isiyo ya Kiotomatiki	Madhara
ATCL	Utoaji wa bili kwa malipo ya mizigo	Uzembe, makosa ya kibinadamu, usumbufu kwa wateja, hatari ya kupoteza mapato.
UCSAF	Kukokotoa Ushuru wa Huduma	Kutegemea kwa Excel kwa mahesabu kunaleta hatari ya viwango vya ushuru visivyo sahihi.
	Ufuatiliaji wa hali ya leseni za mtoa huduma wa mawasiliano na mapato ya jumla yaliyokusanywa	Uwasilishaji usio sahihi wa ushuru na kushindwa kukusanya ushuru kutoka kwa wamiliki wote wa leseni.
TIRA	Mchakato wa bima ya maisha na afya	Kuongezeka kwa uwezekano wa makosa na ucheleweshaji wa kazi.
ATCL	Mchakato wa malipo ya mizigo	huduma za mizigo zingeweza kutolewa bila malipo sahihi, na hivyo kusababisha upotevu wa mapato
	Mchakato wa Kuidhinisha marejesho ya fedha	Kurejesha pesa kwa ucheleweshaji wa uthibitishaji wa mlipwaji ambao huleta makosa na katika malipo.
	Ufuatiliaji wa mizigo iliyosafirishwa	Huathiri uzoefu wa mteja, na kusababisha ucheleweshaji na kutoridhika
REA	Kazi za msingi za taasisi	Mahesabu yanayofanywa na binadamu bila mfumo yanaweza kusababisha Makosa na hasara za fedha, kutokana na kutegemea utendaji wa afisa pekee.
	Ukusanyaji wa ushuru wa huduma	Mahesabu ya kibinadamu yanaweza Kusababisha makosa na hasara za fedha na pia kutokuwepo kwa utaratibu wa kufuatilia madeni ambayo bado hayajalipwa.
LATRA	Kuendesha utaratibu wa kufuta makosa kwa Kutumia teknolojia ya nusu-Kiotomatiki	Hatua za kutegemea kibinadamu /afisa zinachelewesha mchakato, kuongeza



Taasisi	Huduma Isiyo ya Kiotomatiki	Madhara
		makosa, na kupunguza uwezo wa kufuatilia hatua zilizopitishwa, hivyo kuathiri ufanisi.
Idara ya Uhamiaji	Utoaji wa pasi maalum za makazi na pasi za Biashara	Taratibu za kujiendesha zinaweza kusababisha ucheleweshaji, hitilafu, na kutozwa zaidi kwa gharama zinazohusiana.
TPC	Usimamizi wa malipo ya kuchelewesha kuchukua bidhaa pamoja na gharama za usimamizi wa mizigo	inaweza kusababisha upungufu, ukosefu wa usahihi na ucheleweshaji wa utoaji wa bili na utambuizi wa mapato ya taasisi.
	Malipo ya mishahara na malipo ya likizo	uzembe na makosa ya kibinadamu, yanayoathiri shughuli za utendaji kwa ujumla.
